


## **WASIFU WA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

## 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Mahali Ilipo

Wilaya ya Rungwe ni moja ya Wilaya 5 na Halmashauri 7 zinazounda Mkoa wa Mbeya. Aidha ni moja ya Wilaya za zamani hapa nchini kuanzia wakati wa Utawala wa Wajerumani. Wilaya hii iko katika "longitudo 8° 30'E na 9° 30'E na latitudo 33° S na 34° S." Wamissionari wengi wa Madhehebu mbalimbali waliingia katika Wilaya hii mwishoni mwa karne ya 19 wakitokea Malawi ambao pamoja na kueneza Dini wametoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya wananchi hususani katika nyanja za elimu na afya. Makao Makuu ya Wilaya yapo katika Mji wa Tukuyu ambao upo kilomita 72 kutoka Makao makuu ya Mkoa wa Mbeya. Katika mji wa Tukuyu huduma zote muhimu kama za Maji, Elimu, Kituo cha Polisi, Mahakama, Gereza, Masoko, Maduka, Hoteli, kituo cha mabasi na mabenki zinapatikana kwa urahisi. Halmashauri hii inapakana na Halmashauri za Wilaya ya Mbeya upande wa Kaskazini, Halmashauri ya Busokelo upande wa Mashariki, Kyela upande wa Kusini na Ileje upande wa Magharibi.



## ***Mchoro 1: Ramani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe***

## 1.2 Eneo, Utawala na Idadi ya Watu

Eneo la Wilaya ni kilometra za mraba 1,231.86. Kufuatana na maoteo ya Sensa ya Watu na makazi kwa mwaka 2019, Halmashauri ina Watu **302,430** wakiwemo Wanaume **145,035** na Wanawake **157,395**. Halmashauri ina Jimbo moja la Uchaguzi na imegawanyika katika Tarafa 3 zenye jumla ya Kata 29 na Vijiji 99 ambavyo vimeandikishwa. Mgawanyo wa Watu kwenye Tarafa hizo kufuatana na maoteo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2019 ni kama ifuatavyo:-

### Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa watu Kitarafa

Tarafa	Jumla
Tukuyu Mjini	26,652
Ukukwe	202,018
Pakati	73,759
<b>JUMLA</b>	<b>302,430</b>

*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

### Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Kata na Kitarafa

NA	TARAFA	KATA	IDADI YA WATU
1	<b>Tukuyu Mjini</b>	Bulyaga	7,996
		Bagamoyo	3,998
		Msasani	7,729
		Kawetele	6,930
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>26,652</b>
2	<b>Ukukwe</b>	Ibighi	10,442
		Suma	7,340
		Makandana	8,933
		Ikuti	15,294
		Malindo	6,993
		Lufingo	20,141
		Iponjola	
		Nkunga	18,936
		Lupepo	
		Kyimo	16,465
		Kinyala	15,102
		Kiwira	29,620
		Ikama	4,419
		Isongole	21,928
		Ndanto	
		Swaya	8,865
		Masebe	5,828
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>202,018</b>
3.	<b>Pakati</b>	Masukulu	7,217
		Kisiba	8,256
		Masoko	7,643
		Bujela	6,949

	Ilima	8,391
	Kisondela	13,788
	Mpuguso	17,399
	Kikole	4,115
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>69,483</b>
	<b>JUMLA</b>	<b>302,430</b>

Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe (maoteo 2019)

### **1.3 Hali ya Hewa na Kanda za Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo**

Wilaya ya Rungwe ina wastani wa mm 900 hadi mm 2700 za mvua na hali ya joto kati ya 18C na 25C kwa mwaka mzima. Hali hii husababisha kuwa na Kanda kuu tatu za mazao kama ifuatavyo:-

#### **1.3.1 Ukanda wa Juu**

Hizi ni sehemu ambazo ni mfululizo wa milima ya Mporoto katika Kata ya Isongole na inafaa kwa kilimo cha pareto na viazi mviringo.

#### **1.3.2 Ukanda wa Kati**

Hizi ni sehemu zenyenye baridi na zinafaa kwa kilimo cha chai, kahawa, ndizi maparachichi na maharage.

#### **1.3.3 Ukanda wa Chini**

Hili ni eneo lenye joto kusini mwa Wilaya, mpakani mwa Wilaya ya Kyela. Eneo hili linafaa kwa kilimo cha mahindi, mpunga, kokoa, viazi vitamu, mihogo ana aina mbalimbali za mazao jamii ya mikunde.

## **2. MIKAKATI YA SERIKALI YA WILAYA /HALMASHAURI KATIKA KUFIKIA MALENGO YA MKUKUTA**

Wilaya ya Rungwe kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo inatekeleza malengo na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa kuzingatia, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 – 2020.

Aidha, Halmashauri inazingatia mikakati inayowezesha ukuaji wa Uchumi ulio endelevu. Kuweka mazingira muafaka ya ukuaji wa Sekta Binafsi, Ubora na Usawa katika utoaji huduma za jamii; kukuza Utawala Bora na Uwajibikaji, kujumisha masuala ya Jinsia, kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI na kuhifadhi Mazingira. Wilaya inalenga kujenga uchumi endelevu na kuwaandaa wananchi wake kuhimili ushindani.

### **Ili kufikia malengo haya Wilaya imejiwekea mikakati ifuatayo:-**

- i) Kuendeleza, kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja wilayani ili kurahisiha usafiri na usafirishaji wa abiria na bidhaa,
- ii) Kutoa msukumo katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya Kilimo kwa hekta ili kuongeza ufanisi,
- iii) Kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hasa katika usindikaji wa mazao ya kilimo kama chai, ndizi, maziwa, mananasi, maparachichi ili kuyaongezea thamani,
- iv) Kuwasaidia wakulima kutafuta masoko ya bidhaa zao kwa kuwaunganisha na wafanyabiashara walio nje ya Wilaya ili kupata bei nzuri ya mazao ya kilimo kama ndizi, maparachichi, chai, mananasi kwa lengo la kuongeza tija kwa wakulima,
- v) Kuwaunganisha wakulima na Taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo ili kuwakopesha wananchi kupata pembejeo za kilimo kwa urahisi na kuwahamasisha wajunge na vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) katika maeneo yao,
- vi) Kuboresha Sekta ya Elimu kwa kujenga miundombinu iliyo bora katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ili kuwaandaa wananchi kuweza kuhimili ushindani katika soko la ajira,
- vii) Kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali kupidia ada, leseni kodi za majengo na gawio kutokana na faida katika makampuni ambayo Halmashauri ina hisa na ushuru wa huduma kutoka kwenye makampuni yanayotoa huduma Wilayani na
- viii) Kuimarishe utoaji wa huduma bora za afya ili kuwa na wananchi wenyе afya na wanaoweza kufanya kazi na kuchangia uchumi wao, Wilaya na Taifa kwa ujumla.

### **3. HALI YA MAENDELEO YA WILAYA KISEKTA**

#### **3.1 Sekta ya Kilimo**

Kutokana na hali nzuri ya hewa, Sekta ya Kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Wilaya. Zaidi ya asilimia 90 ya pato lote la Wilaya linatokana na Kilimo. Sekta nyingine ni pamoja na mifugo, Biashara na Maliasili. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 92,389.5. Wilaya inatilia mkazo ongezeko la uzalishaji kwa hekta kutokana na maeneo madogo yaliyopo kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Kuhifadhi Ardhi, Maji na Mazingira. Kwa mwaka 2019/20 Halmashauri ilikadiria kuzalisha mazao ya chakula tani 1,316,324.8, mpaka sasa kiasi kilichozalishwa ni tani 1,053,059.8 sawa na asilimia 80; Kwa mazao ya biashara makadirio ya uzalishaji yalikuwa tani 9,262.3, wakati kiasi kilichozalishwa ni tani 7,536.9 sawa na asilimia 81.4 ya lengo lililokusudiwa. Mikakati iliyopo ya kuongeza uzalishaji ni pamoja na kuongeza huduma za ugani, kudhibiti

visumbufu vya mazao, kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao kupitia mashamba darasa na kuongeza matumizi ya mbegu bora na mbolea.

Mazao makubwa ya biashara ni kahawa, chai na kokoa. Mazao ya chakula ni pamoja na ndizi, mahindi, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage na mpunga. Aidha uzalishaji wa zao la kahawa umekuwa ukishuka na kupanda. Kupanda na kushuka kwa uzalishaji wa kahawa umechangiwa na ukosefu wa mikopo ya pembejeo, ukosefu wa soko la kuaminika na bei ndogo anayolipwa mkulima ukilinganisha na gharama za uzalishaji. Kwa upande wa mazao ya chai na kokoa, uzalishaji umekuwa ukiongezeka kutokana na uhakika wa soko kwa miaka ya karibuni. Uzalishaji wa kahawa, kokoa na chai kwa kipindi cha miaka 5 (2015/2016– 2019/2020) ni kama inavyooneshwa katika jedwali la hapo chini:-

#### **Jedwali Na. 3: Uzalishaji wa mazao makuu ya Biashara katika Tani**

<b>Na</b>	<b>Mwaka</b>	<b>Kakao</b>	<b>kahawa</b>	<b>Chai</b>
01	2015/2016	654	291.6	7,877.8
02	2016/2017	688	608	7,961
03	2017/2018	532.9	656.1	8,109.5
04	2018/2019	407.2	664.4	7,437.5
05	2019/2020	520	647.7	6,369.2

**Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya, 2019/20 kuishia Juni 2020**

#### **3.1.1 Wastani wa Uzalishaji wa Mazao kwa Hekta.**

Viwango vya uzalishaji kwa hekta vilivyokadirwa kiwilaya vimekuwa havifikiwi kutokana na sababu au matatizo mbalimbali ikiwemo wakulima kutozingatia kanuni za kilimo bora na matumizi ya pembejeo. Wilaya inaendelea kutoa elimu juu ya uzingatiaji wa kilimo bora. Jedwali lililopo hapo chini linaonyesha hali halisi ya uzalishaji wa mazao ya chakula.

#### **Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa mazao makuu ya chakula (Tani) mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020**

<b>N a</b>	<b>Mwaka/ Mazao</b>	<b>2015/201 6</b>	<b>2016/201 7</b>	<b>2017/201 8</b>	<b>2018/201 9</b>	<b>2019/202 0</b>
1	Mahindi	103,737	103,900	95,940	64,881	98,705
2	Ndizi	356,404	357,200	300,236.2	315,149	294,605
3	Viazi Mviringo	503,119	503,119	511,056	343,945	503,119
4	Mpunga	3,023	3,050	2,780	747.0	3,050
5	Maharag we	22,071	22,077	22,831.6	18,034.8	441.5

**Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya, 2019/2020**

### **3.1.2 Hali ya Chakula Wilayani**

Wilaya hii haina matatizo makubwa ya ukosefu wa chakula kwa ujumla. Hii inatokana na hali nzuri ya hewa na mvua za kutosha zinazowezesha kulima karibu mwaka mzima. Chakula kikuu kwa wakazi wengi ni ndizi, zao ambalo linalimwa sehemu kubwa ya Wilaya. Vile vile upatikanaji wa vyakula vingine kama viazi mviringo, viazi vitamu na mihogo unapunguza matatizo ya ukosefu wa chakula.

### **3.1.3 Mahitaji ya Pembejeo**

Wastani wa tani 16,019 za mbolea ya Viwandani huhitajika kila mwaka kwa ajili ya uzalishaji wa mazao mbalimbali. Katika msimu wa kilimo 2019/2020 kiasi cha tani 8,692 za mbolea sawa na 54% ya mahitaji zilitumika katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Aidha tani 17.4 za madawa ya unga zilitumika kwa msimu huo kati ya tani 22.7 sawa na 76.7% zilizokuwa zinahitajika. Pia, lita 23,800.8 za madawa ya maji zilitumika na wakulima katika kilimo kati ya lita 39,668 sawa na 60% zilizokuwa zikihitajika. Matatizo yaliyopo ni bei ya mbolea na madawa kwa mkulima kuwa juu ikilinganishwa na uwezo wao wa kununua. Kampuni ya Chai (Wakulima - WATCO) huagiza mbolea na madawa na kuwakopesha wakulima. Kutokana na upungufu wa mbolea na madawa unaojitokeza na bei kuwa kubwa, mkazo unatiliwa katika matumizi ya samadi itokanayo na mifugo pamoja na mboji.

### **Jedwali Na. 5: Matumizi ya Zana na Pembejeo za Kilimo 2015/16 -2018/19**

Mwaka	Mbolea za Chumvichumvi(Tani)				Madawa ya Kudhibiti visumbufu(Lita)			
	Mahitaji	Iliyopati kana	% ya upatik anaji	Pungufu	Mahitaji	Iliyo patikana	% ya Upatik anaji	Pungufu
2015/2016	14,426	13,572.8	94	853.2	36,953	15,211.4	41.2	21,742
2016/2017	14,925	13,230.8	88.6	1,694.2	37,232	16,285.1	43.7	20,947
2017/2018	15,323.3	13,791.2	90	1,532.1	37,778	17,358.1	45.9	20,420
2018/2019	16,019	8,692	54	7,327	39,668	23,800.8	60	15,867
2019/2020	16,000	12,960	81	3,040	40,189	28,132	70	12,057

**Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W),  
2019/2020 kuishia Juni.**

**Jedwali Na. 6: Matumizi ya Zana na Pembejeo zingine za Kilimo  
2015/16 - 2019/2020**

NA	MWAKA	MBEGU BORA (KWA TANI)			MAKISAI ( KWA IDADI)		
		MAHITA JI	ZILYOPATI KANA	UPU NGUFU	MAHITAJ I	YALIYO PATIKANA	UPUNGUF U
01	2015/2016	288	240	48	625	466	159
02	2016/2017	290.0	261	29	625	612	13
03	2017/2018	267.8	241	26.8	630	622	8
04	2018/2019	296.2	266.6	29.6	630	618	12
05	2019/2020	298.0	268.2	29.8	630	620	10

**Chanzo: Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya,  
2019/2020.**

### **3.2 Sekta ya Mifugo**

Wakazi wa Rungwe hufuga mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo nguruwe kuku na bata. Aidha ng'ombe wa kisasa ndio wanaofugwa kwa wingi kutokana na hali ya hewa ya ubaridi, mvua za kutosha kwa kipindi kirefu cha mwaka na kutegemeana kwa zao la ndizi na mbolea ya ng'ombe katika kuzalisha ndizi na parachichi. Kuenea kwa ng'ombe wa kisasa kumechangiwa na ushirikano wa wadau mbalimbali kama Heifer international project, TASAF, DADPS, Africa bridge, East Africa dairy development project, ASAS dairy company, Africa dairy genetic project na uwepo wa kituo cha Utafiti wa mifugo Uyole. Hivi sasa Halmashauri ina jumla ya ng'ombe wa kisasa 40,826 (kwa mujibu wa sensa ya April, 2019) na uzalishaji wa maziwa umefikia lita 44,758,989 kwa mwaka sawa na wastani wa lita 146,750 kwa siku na wastani wa uzalishaji kwa ng'ombe kwa siku ni lita 10 hadi 15. Kiasi kinachouzwa kwenye soko rasmi ni Lita 21,100 kwa siku sawa na 11% ambapo nusu ya maziwa yananunuliwa na Kampuni ya ASAS DAIRY COMPANY (10,000) kwa siku. Kiasi kikubwa cha maziwa huuzwa kwenye soko lisilo rasmi kutokana na wafugaji wengi kutokubaliana na bei ya maziwa ya Tsh 600 hadi 650 kwa lita.

Aidha ili kuboresha soko la maziwa na mfumo wa ununuzi wa maziwa Mradi wa EADD umeviwezesha Vyama vya Msingi 22 kuunda Chama kikuu cha Ushirika (MAZIWA COOPERATIVE UNION) na kukiwezesha kujenga vituo 10 vya kisasa vya kupokelea maziwa kwa kila kituo kuwa na tenki pamoja na jenereta, vituo vimekamilika na uwezo wa kukusanya lita 34,000 kwa siku 1, kwa sasa vituo 06 vimefunguliwa amabapo Mnunuzi wa maziwa kwenye vituo hivyo ni ASAS Dairy company.

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Mifugo inayofugwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe**

Aina ya Mifugo	Idadi ya Mifugo
Ng'ombe wa asili	8,374
Ng'ombe wa kisasa	40,826
Mbuzi wa asili	7830
Mbuzi wa kisasa	240
Kondoo	735
Nguruwe	16,510
Kuku wa asili	215,120
Kuku wa kisasa	1560
<b>Jumla</b>	<b>291,195</b>

**Chanzo: Idara ya Mifugo na Uvuvi Wilaya Rungwe 2019/2020**

**CHANGAMOTO**

Changamoto zinazoikabili sekta hii ni pamoja na:

1. Upatikanaji wa soko la maziwa lenye tija kwa mfugaji (kwa sasa bei ya lita moja ya maziwa ni Tsh 600 hadi 650).
2. Upungufu wa maafisa ugani. Kwa sasa Halmashauri ina upungufu wa maafisa ugani 97. Wataalam wa mifugo waliopo ni 24 tu na ikama inaelekeza kuwa ngazi ya wilaya wawepo 08 na kwenye kata na vijiji awepo mtaalam mmoja mmoja mmoja.
3. Uchakavu wa miundo mbinu ya machinjio.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

1. Halmashauri inaendelea kuwashawishi wajasiriamali kuendelea kuwekeza katika biashara ya maziwa kwani hadi sasa wapo wajasiliamali wenye viwanda vidogo 08 na vyama vya wafugaji 02 vinavyo sindika maziwa. Aidha, Kampuni ya ASAS inayonunua maziwa mabichi na kupeleka Iringa Imejenga Kiwanda cha kusindika Maziwa na Kimekamilika na kitakuwa na uwezo wa Kusindika lita 50,000 kwa siku. Kiwanda hiki kikikamilika kitaweza kupunguza changamoto ya soko la maziwa.
2. Kufuatia upungufu wa wataalamu wa ugani, Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri wataalamu wa Mifugo 15 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na pia wadau wengine wa mifugo (East Africa dairy project, ASAS DAIRIES na Africa Bridge) wameajiri maafisa ugani 03 na kutoa mafunzo kwa wagani kazi 42 ambao husaidiana na maafisa ugani wa Serikali kutoa elimu na tiba kwa mifugo.

**3.** Ili kuboresha machinjio, Halmashauri imetenga 10,000,000 kwa mwaka 2020/2021 kurekebisha mitaro ya miundombinu ya machinjio ya Kiwira, na Kawetele.

#### **4. Jedwali Na. 8: Maendeleo ya Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020**

Mwaka	Uzalishaji wa Maziwa(lita)	Uzalishaji wa Nyama (Kgs)	Idadi ya wafugaji waliopatiwa mafunzo
2015/2016	60,070,000	1,458,235	5,800
2016/2017	62,000,000	1,645,790	2,751
2017/2018	62,500,000	1,347,555	1,582
2018/2019	44,758,989	1,503,844	8,514
2019/2020	44,758,989	995,040	11,210

**Chanzo: Idara ya Mifugo Wilaya, 2019/2020**

#### **3.3 Sekta ya Elimu Msingi**

Lengo kuu la Sekta ya Elimu ni kusimamia shughuli za elimu iliyo katika mfumo rasmi na isiyo katika mfumo rasmi kwa shule za msingi na vituo vya ufundis stadi. Lengo ni kuboresha Elimu na Mafunzo kwa kuimarisha programu ya mafunzo kazini, kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na kukarabati miundombinu ya shule. Aidha, Sera ya Elimu inasisitiza kushirikisha jamii katika kuendesha na kuziongoza shule. Sekta hii inasimamia huduma muhimu zifuatazo:-

##### **3.3.1. Malengo na Mikakati 2017- 2020**

- Kuandikisha Watoto wenyewe umri wa kwenda shule kutoka asilimia 70.5 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2019.
- Kupunguza uwiano wa vitabu vya kiada wa 1: 3 hadi kufikia 1:2 ifikapo mwaka 2018
- Kuungeza nyumba za walimu kutoka 274 zilizopo hadi kufikia nyumba 300 ifikapo mwaka 2020.
- Kuungeza idadi ya madarasa kutoka 958 yaliyopo hadi 1,510 ifikapo mwaka 2020
- Kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwa wanafunzi wanaohitimu elimu ya Msingi kutoka asilimia 0.1 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 0 ifikapo 2020.

##### **3.3.2. Utekelezaji wa Malengo na Mikakati ya Sera ya Elimu**

###### **3.3.2.1. Elimu ya Awali**

Sera ya Elimu ya mwaka 1995, inaelekeza kuwa kila Shule ya Msingi iwe na Shule ya Awali. Hadi mwaka 2020, Halmashauri ina shule za Msingi 142 shule zote 142 zina madarasa ya awali. Pia kuna madarasa mengine ya

awali 22 yanayoendeshwa na Taasisi mbalimbali kama vile Madhehebu ya Dini, Mamlaka za Chai, Vijiji na Watu binafsi.

### **3.3.2.2. Elimu ya Msingi na Uandikishaji Wanafunzi**

Hadi kufikia Juni, 2020, Halmashauri ina shule za msingi 142 zenyе jumla ya wanafunzi 51,330 wakiwemo wavulana 25,886 na wasichana 25,444. Hali ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la 1 mwaka 2020 ni watoto 6,809 wakiwamo wasichana 3,381 na wavulana 3,428. Lengo lilikuwa ni kuandikisha watoto 6,381.

Mahitaji ya walimu ni 1,639 waliopo ni 1,461 sawa na asilimia 89 wakiwemo wanaume 693 na wanawake 768, kukiwa na upungufu wa walimu 178 sawa na asilimia 12.

### **3.3.2.3. Mwenendo na Ufaulu wa Mitihani ya Darasa la VII**

Katika kipindi cha 2016 hadi 2019 mwenendo wa ufaulu wa wanafunzi wanaomiliza darasa la saba ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

#### **Jedwali Na. 9: Hali ya Ufaulu wa Mitihani ya Darasa la Saba (2016 – 2019)**

Mwaka	Waliofanya Mitihani			Waliofaulu			Waliochaguliwa			Wasiochaguliwa		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	W V	WS	JML
2016	3,025	3,702	6,727	1,920	2,227	4,147	1,920	2,227	4,147	-	-	-
2017	3,275	3,893	7,168	2,258	2,678	4,927	2,258	2,678	4,927	-	-	-
2018	3,411	3,854	7,265	2,460	2,948	5,408	2,460	2,948	5,408	-	-	-
2019	2919	3317	6236	2517	2934	5451	2517	2934	5451			

**Chanzo: Idara ya Elimu ya Msingi, Mwaka 2019**

### **3.3.2.4. Madarasa**

Mahitaji ya madarasa ya kudumu katika Wilaya ni 1,510. Madarasa ya kudumu yaliyopo ni 990, upungufu wa madarasa 520. Wilaya ina mpango kujenga madarasa kwa kushirikisha nguvu za wananchi, wadau wa elimu na serikali kila mwaka, ili kuondoa tatizo hilo ifikapo mwaka 2020.

### **3.3.2.5. Nyumba za Walimu**

Mahitaji ya nyumba za walimu ni 1,639, nyumba zilizopo ni 276 na upungufu ni nyumba 1,363. Wilaya ina mpango wa kujenga nyumba 10 kila mwaka ikishirikisha nguvu za wananchi ili kuondoa tatizo la walimu kukosa nyumba za kuishi ifikapo 2020.

### **3.3.2.6. Vyoo**

Ili kukidhi mahitaji ya vyoo katika shule za msingi, matundu 2,490 yanahitajika. Matundu yaliyopo ni 1,915 na hivyo kuwepo kwa upungufu wa matundu 575.

### **3.3.2.7. Madawati**

Hivi sasa shule zina madawati 19,652 ikilinganishwa na mahitaji ya madawati 17,952 na hivyo kufanya kuwa na ziada ya madawati 1,670.

## **3.4 Elimu ya Sekondari**

### **3.4.1. Shule za Sekondari**

Halmashauri ina jumla ya Shule za Sekondari 42 zikiwemo shule 32 za Serikali. Zilizobaki kumi (10) zinamilikiwa na Taasisi binafsi na mashirika ya kidini.

#### **3.4.1.1 Mahitaji ya Vyumba vya Madarasa**

Mahitaji ya madarasa ya kudumu katika Halmashauri ni 480. Madarasa ya kudumu yaliyopo ni 455, hivyo kuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 25.

#### **3.4.1.2 Nyumba za Walimu**

Mahitaji ya nyumba za walimu ni 805. Nyumba zilizopo ni 93 na upungufu ni nyumba 731. Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa maendeleo itaendelea kujenga nyumba za walimu ili kukidhi mahitaji.

#### **3.4.1.3 Matundu ya Vyoo**

Ili kukidhi mahitaji ya vyoo katika shule za Sekondari, matundu 846 yanahitajika. Matundu yaliyopo ni 835. Upungufu uliopo ni matundu 11. Hata hivyo kwa ngazi ya shule kuna baadhi ya shule zina matundu ya ziada ya vyoo. kwa kushirikiana na wananchi, Halmashauri inaendelea kujenga matundu zaidi ya vyoo ili kukidhi mahitaji.

#### **3.4.1.4 Meza na Viti**

Hivi sasa shule zina samani zilizopo 18,634, mahitaji ni kuwa na samani idadi ya 19,118. Sera ya elimu Kitaifa ni mwanafunzi 1 kwa meza na kiti 1. Wilaya kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wamefanikiwa kutengeneza samani za shule ili kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

### **3.4.1.5 Mahitaji ya Maabara na Samani Zake kwa Shule za Serikali**

Mahitajji ya vyumba nya maabara ni vyumba 96, vyumba vilivyopo nya maabara ni 88 sawa na upungufu wa vyumba 8. Halmashauri inaendelea kushirikiana na wadau wa elimu kumaliza upungufu wa vyumba hivyo.

### **3.4.2 Vyuo**

#### **3.4.2.1 Vyuo nya Kitaifa.**

Vipo sita ambavyo ni nya mafunzo ya Ualimu (2), Huduma za Akina Mama na Watoto (PHNS) (1), Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (1), Chuo cha Magereza Kiwira na chuo cha Teknolojia rahisi ya matengenezo ya barabara -ATTI (1).

#### **3.4.2.2 Vyuo nya Ufundu Stadi.**

Vipo vyuo nya Ufundu Stadi 8 nya binafsi ambavyo vinasaidia vijana kujiajiri wenyewe baada ya kuhitimu mafunzo yao.

### **3.5. Sekta ya Afya**

#### **3.5.1. Utoaji wa Huduma za Afya**

Halmashauri ina Hospitali 2 ikiwa 1 ya Serikali na 1 ya dini, vituo nya Afya 4, kati ya hivyo , nya Serikali ni 2 na cha madhehebu ya dini ni 2. Kwa pamoja Hospitali na Vituo nya Afya vina vitanda 455. Aidha, zipo zahanati 42 kati yake 35 ni za Serikali na 7 ni za Madhehebu ya Dini na watu binafsi.Wastani wa umbali wa Zahanati toka kwa mtu aliye mbali na huduma hiyo ni kilomita 6.7. Kitaifa, wastani kwa mtu aliye mbali na huduma hiyo ni k.m. 10. Wilaya ya Rungwe imevuka lengo la Kitaifa kwa kutoa huduma za Afya karibu zaidi na Wananchi. Uwiano wa huduma za Afya kwa wananchi ni 1:5,375.

Vituo vyote vinasimamiwa na Kamati za Uendeshaji chini ya Bodi ya Huduma ya Afya ya Wilaya, Bodi hii ilianzishwa rasmi Julai, 2004.

#### **3.5.2 Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI**

Wilaya ya Rungwe hivi sasa ina wastani wa maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa asilimia 9.2% kutoka asilimia 9% mwaka 2016. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hili Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inaendelea na mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kwa kutoa elimu ya afya dhidi ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU. Elimu hii endelevu inatolewa kwa njia ya vikao mbali mbali nya kudhibiti UKIMWI kwa ngazi ya Halmashauri (CMAC), ngazi ya Kata (WMAC) na ngazi ya vijiji (VMAC) na kwenye vituo vyote nya kutolea huduma za afya vilivyopo katika Halmashauri yetu, pia kwa kutumia fursa za Redio za ndani zilizopo Wilayani (Radio Chai na redio Rungwe FM), makundi mbali mbali ya waelimisha rika, Wahudumu wa afya

majumbani, Watu maarufu katika jamii, watu waiishio na maambukizi ya VVU na vikundi mbalimbali vya hamasa.

Pamoja na huduma hiyo, Halmashauri hutoa huduma ya kutoa ushauri nasaha na kupima damu kwa hiari, kuitia vituo 50 vinavyotoa huduma hiyo. Ambavyo kati ya hivyo 43 ni vya serikali, 5 ni vya mashirika ya kidini na 2 ni watu binafsi.

Aidha Halmashauri hutoa huduma ya tiba kwa watu ambao tayari wamekwishapata maambukizi ya VVU/UKIMWI. Kwa kushirikiana na Wahisani mbalimbali tumeboresha huduma za VVU kwa kuongeza vituo 8 vya tiba na matunzo, kutoka vituo 13 tulivyo kuwa navyo mwaka 2018 hadi kufikia **vituo 21 mwaka 2019**. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuna jumla ya wagonjwa **10,612** wanaishi na maambukizi ya VVU walioko kwenye huduma za tiba na matunzo, tangu huduma hizi zilipoanzishwa mwaka 2003 katika Halmashauri yetu, kati ya hao wanaume ni **3,950** sawa na asilimia **36%** ya wagonjwa wote, na wanawake ni **6,662** sawa na asilimia **64%** ya wagonjwa wote.

### **3.6. Sekta ya Maji**

#### **3.6.1 Hali ya Maji Vijijini**

Halmashauri inafanya jitihada za kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salama karibu na makazi yao ndani ya umbali wa mita 400 kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya maji ya mwaka 2002. Asilimia 67.7 ya wananchi waishio Vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama sawa na watu 162,750 kati ya watu wapatao 240,250 waishio maeneo ya Vijijini.

Miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa na Serikali katika Halmashauri yetu ni miradi ya maji ya Vijiji 12 chini ya mpango maendeleo ya sekta ya maji (WSDP). Miradi hiyo inatekelezwa katika Vijiji vya Syukula, Katabe, Kyimo, Simike, Lugombo, Nkunga, Itete, Kapugi, Ijigha, Masukulu, Isyonje, Ilolo na Lukata. Pia kuna miradi mingine mikubwa miwili ya Mwakaleli 1 na Masoko iliyoanza kutekelezwa mwaka 2010 na inaendelea kutekelezwa hadi sasa kutokana na usimamizi na uratibu mbaya wa Mhandisi Mshauri huko nyuma pamoja na ufinyu wa bajeti inayotengwa kila mwaka. Aidha miradi hii ikikamilika itawezesha asilimia **86** ya wananchi wa Halmashauri hii kupata maji safi na salama ambayo ni sawa na wakazi wapatao 208,868 katika Vijiji 30. Miradi hiyo ina jumla ya thamani ya TSh. **17,833,682,441.77.**

### **3.6.2 Maji Mjini**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tukuyu ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa tarehe 21/08/2002 na ilitangazwa kwenye gazeti Namba 258 kuwa Mamlaka ya daraja C. Lengo la kuanzishwa kwa Mamlaka ni kwa ajili ya kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa mji wa Tukuyu. Baada ya Mamlaka kuanzishwa ilianza kuhudumia wakazi wa mji wa Tukuyu kwa kupitia mifumo ya maji iliyopo ambayo ilijengwa kipindi cha miaka ya 1957 na 1960 ambayo ndiyo mifumo ya maji inayotumika hadi sasa katika Kata 6 ambazo ni Makandana, Kawetele, Ibighi, Bulyaga, Bagamoyo na Msasani zenyne wakazi wapatao 50,926. Asilimia 80 ya wakazi hao wanapata maji safi na salama sawa na wakazi wapatao 40,741.

Uzalishaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji vilivyopo ni mita za ujazo **5,538** kwa siku wakati wa kiangazi na 6,073 kwa siku wakati wa masika na mahitaji halisi ni mita za ujazo **6,318** kwa siku ikiwa ni pungufu ya mita za ujazo zipatazo 780 kwa siku. Asilimia 43 ya wakazi wanapata huduma ya maji kwa masaa 24 na asilimia 57 wanapata huduma ya maji kwa mgao wa wastani wa masaa **17** kwa siku.

Juhudi za kuimarisha na kupanua huduma ya maji zitaendelezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Halmashauri kwa kujenga matanki matano (5) ya kuhifadhi maji pamoja na vyanzo viwili vingine vya maji ili kuongeza masaa ya upatikanaji wa maji pamoja na mtandao wa kusambaza maji ili kukabiliana na ongezeko la watu.

## **3.7. Sekta ya Maliasili na Hifadhi ya Mazingira na Ardhi.**

### **3.7.1 Maliasili**

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inakadirwa kuwa na jumla ya hekta 16,009.87 za misitu ya hifadhi na hekta 7,341 za misitu ya kawaida. Sehemu kubwa ikiwa ni misitu ya kupandwa. Misitu ni chanzo kikubwa cha nishati na kuwa chanzo cha kuleta mvua katika maeneo yenyne misitu katika wilaya yetu. Matumizi mengineyo kutohana na mazao ya misitu ni pamoja na mbao na nguzo.

Wastani wa mahitaji ya nishati katika Halmashauri ni mita za ujazo **360,000** kwa mwaka. Mahitaji ya kuni na mkaa ni 98% ya mahitaji yote ambapo mbao na nguzo zinachukua 2% au mita za ujazo **7,200**. Halmashauri ina uwezo wa kutoa nishati ya wastani wa mita za ujazo **200,000**, kiasi kinachoonyesha kuwa kuna ukataji ovyo wa miti ili kufidia upungufu wa mita za ujazo **160,000**.

### **3.7.2 Hifadhi ya Mazingira**

Halmashauri ina lengo la kupanda miti **1,600,000** kila mwaka, lengo hili linafikiwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa uhifadhi mazingira (NGOs), Taasisi na wananchi. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya miti **1,819,000** imepandwa katika Kata zote 29 za Halmashauri, maeneo ya Taasisi na mashamba ya watu binafsi.

Ili kukabiliana na changamoto za kimazingira kwa ngazi ya chini, Halmasahuri imeunda Kamati za kuhifadhi mazingira za Kata 29 na Vijiji 125 na kazi yake ni kuimarisha utunzaji wa mazingira katika maeneo yao sambamba na kuhimiza upandaji wa miti ya asili.

### **3.7.3 Utalii**

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ni moja kati ya Wilaya chache zenye vivutio vya utalii vingi na vya kipekee. Vivutio vya utalii ni chanzo cha mapato kwa Hamashauri na wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Vivutio vya utalii vya kipekee vinavyopatikana Wilaya ya Rungwe ni Daraja la Mungu, Kijungu, Mti wa kipekee wa Mvule, Mlima Rungwe, Maziwa yanayopatikana katika vilele vya milima (ziwa Ngozi, ziwa Kisiba, ziwa Ndвати, ziwa Ilamba, Itamba, n.k) chemichemi za maji moto na Maporomoko ya maji ya Kapologwe, Malasusa na Malamba. Halmashauri imeandaa mpango mkakati utakaowashirikisha wadau wa utalii ili kukuza shughuli za utalii Wilayani Rungwe ili ziweze kuleta tija kiuchumi na zichangie pato la Taifa.

Juhudi za kuvitangaza vivutio hivi zinaendelea kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali kama wakala wa huduma za misitu Tanzania (TFS), SPANEST na TANAPA, pamoja na wadau mbalimbali wa utalii kama waandishi wa habari, Kampuni za kitalii, NGOs (AWF,WCS n.k ). Kamati ya utalii ya Wilaya imeundwa na imeandaa mkakati wa miaka mitano (2015-2020) wenye lengo la kukuza na kuendeleza sekta ya utalii Wilaya ya Rungwe.

### **3.7.4 Ardhi**

Ardhi iliyopo Wilayani haitoshi kwa mahitaji muhimu ya wakulima kwa misingi kwamba ni 8% tu ya vijiji vyote Wilayani vilivyo na ardhi kubwa zaidi ya Ha. 150. Lipo tatizo kubwa la kugombea mipaka kati ya vijiji na vijiji kutokana na ongezeko la watu. Juhudi za kuwapa hati miliki za mila wananchi zinaendelea baada ya Vijiji vyote kupimwa.

## **3.8. Viwanda na Biashara**

### **3.8.1 Viwanda**

Halmashauri ya Wilaya ina jumla ya viwanda **3** vikubwa, viwanda **3** vya kati viwanda **124** vidogo na viwanda vya kati vinavyojengwa **2**. Kutokana na fursa zilizopo, Halmashauri ina malengo ya kuanzisha viwanda vya

matunda, maziwa, Viazi (crips), kiwanda cha chakula cha mifugo, machinjio ya ng'ombe, Soko la ndizi, soko la viazi mviringo na kiwanda cha kusaga kahawa na kokoa.

Ili kuongeza soko kwa bidhaa zinazopatikana Wilayani, Halmashauri inaendelea na jitihada ya kutafuta maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa soko/kiwanda ambapo kwa kushirikiana na wadau lengo la uboreshaji wa huduma kwa kuanzisha viwanda litatimia. Maeneo yanayotafutwa ni kama yafuatayo:-

- Maeneo yanayomilikiwa na Serikali kama Serikali ya Kijiji, Halmashauri n.k
- Maeneo ambayo Serikali inaweza kuyamiliki kwa kununua au kulipa fidia.
- Maeneo yanayomilikiwa na wananchi ambao wapo tayari maeneo yao yatumike kwa uwekezaji kwa makubaliano maalum.

Hadi kufikia Juni 2019, Maeneo yaliyopatikana kwa ajili ya uwekezaji ni:-

#### **Jedwali Na. 10: Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Uwekezaji**

N A	ENE O LIL IPO  (KIJ IJI)	UM ILI KI	UK UB WA WA ENE O	A INA YA MAT U MIZ I YAN AY OPEN DE KE Z WA
1.	Kijiji cha Ilenge jirani na ATTI	Halmashauri	Ekari 10.67	Soko la ndizi
2.	Kijiji cha Ilenge eneo lililotolewa na TANROAD	Halmashauri	Ekari 2	Kiwanda cha kati cha kusaga kahawa na kokoa
3.	Kijiji cha Ilenge kituo cha Rasilimali ya wakulima	Halmashauri	Ekari 15	Kiwanda cha kati cha maziwa
4.	Kijiji cha Unyamwanga	Halmashauri	Halijapimwa	Kiwanda cha kati cha crips (Viazi)
5.	Kijiji cha Mbeye I	Binafsi	Ekari 3	Soko/ kiwanda cha viazi
6.	Kijiji cha Ilundo	Serikali ya Kijiji (Hati)	Ekari 38	Ufugaji wa samaki
7.	Kijiji cha Ilundo	Serikali ya Kijiji(Hati)	Ekari 9	Soko la ndizi

#### **3.8.2 Biashara**

Wilaya ya Rungwe kama Wilaya zingine za Mkoa wa Mbeya inao wafanyabiashara ambao hutoa huduma za mahitaji mbalimbali yatokanayo na viwanda na kilimo kwa wananchi. Wilaya ina jumla ya wafanyabiashara

8964 ambapo wafanyabiashara **1222** ni biashara ambazo zimesajiliwa na ziko rasmi na wafanyabiashara **7742** ni biashara ndogondogo zisizo rasmi.

Mkakati wa Halmashauri ni kuboresha vituo vya kufanya biashara vilivyopo na kutafuta masoko mapya ili kumsaidia mzalishaji hasa wa mazao ya Kilimo na Mifugo kuuza kwa bei nzuri ambayo itamuongezea kipato.

### **3.9. Sekta ya Ushirika**

Halmashauri ya Rungwe ina historia ndefu ya harakati za Vyama vya Ushirika hata kabla ya Uhuru. Vyama hivi vinasaidia sana kukuza uchumi na ustawi wa wakazi wake. Hadi kufikia mwezi April 2020 kulikuwa na vyama vya ushirika **120**. Kati ya hivyo vyama **40** ni vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), **50** ni vyama vya Ushirika wa Mazao (AMCOS), **26** vya wafugaji na **4** ni vyama vya uvuvi na vyama vikuu **2**. Kwa sasa mchango wa vyama vya Ushirika wa Mazao ni kidogo sana na mkazo umekuwa kwenye SACCOS. SACCOS zilizopo Halmashauri ya Rungwe ni **40** zenye wanachama **13,962** hisa shilingi Tshs.**515, 197,210.00**, Akiba shilingi **2,069,102,451**, na Amana shilingi **832,990,847**. Hadi kufikia Machi, 2020, mikopo iliyotolewa kwa wanachama imefikia shilingi **15,231,731,164.00** na iliyorejeshwa ni Tshs.**13,142,270,672.00** sawa na asilimia 86.3 ya marejesho yote na mikopo iliyobaki kurejeshwa ikiwa ni Tshs.**2,089,460,492.00**

### **3.10. Madini**

Sekta ya madini siyo sekta tegemezi hapa Wilayani. Ni machimbo ya gesi yaliyopo Kijiji cha Ikama yanayochimbwa na Kampuni ya Tanzania Oxgen Limited (TOL), na ndiyo madini pekee yanayochimbwa hapa wilayani. Machimbo mengine yanayopatikana Halmashauri ya Rungwe ni pamoja na mchanga, mawe na kokoto.

### **3.11. Uvuvi**

Sekta ya Uvuvi ni ndogo sana hapa Wilayani. Uvuvi unafanywa kupitia mabwawa ya watu binafsi yaliyojengwa karibu na maeneo ya Makazi yao na mabwawa ya asili ya Volkano na mito. Halmashauri ina mabwawa ya samaki 250 na vikundi 7 vya wafugaji wa samaki. Uzalishaji ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

<b>MWAKA</b>	<b>UZALISHAJI KWA KG</b>
2015/2016	1,200
2016/2017	2,400
2017/2018	3,180
2019/2020	3,292

### **3.12. Maendeleo ya Jamii**

Idara ya Maendeleo ya Jamii inendelea kuwahamasisha wananchi katika kujiletea maendeleo endelevu kwa kujiunga katika vikundi vya kiuchumi ili waweze kujikomboa. Mpaka sasa zimeundwa kampuni mbili za VICOBA kama vikundi vinavyojihusisha na mambo ya uchumi. Kampuni hizo ni Tukuyu VICOBA Micro finance Company LTD inayojihusisha na huduma za kifedha mionganini mwa jamii na Balimi VICOBA Micro finance Company LTD ambayo licha kujihusisha na huduma za kifedha inajihuhsisha pia na biashara ya mazao likiwemo zao la chai. Pia Idara inaendelea na utekelezaji wa kupambana na ukatili wa jinsia dhidi ya wanawake na watoto na kudhibiti UKIMWI kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali ya KIHUMBE, JSI na Africa Bridge.

Aidha, Halmashauri imeendelea kuchangia Mfuko wa Wanawake na Vijana kupitia mapato ya ndani na kukopesha vikundi mbalimbali. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuishia Juni, Halmashauri ilitoa mikopo isiyokuwa na riba yenye jumla ya Sh. 483,000,000/- kwa Vikundi 87, ambapo vikundi vya Wanawake 44, Vijana 41 na Watu Wenyewe Ulemavu 2.

## **4. HUDUMA ZA KIUCHUMI NA MAWASILIANO**

### **4.1 Barabara**

Usafiri kwa njia ya barabara Wilayani ni wa kuridhisha isipokuwa kwa sehemu chache zenyetelezi ambapo barabara ni za udongo mtupu bila changarawe. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 725.93 Katil ya hizo kilomita 2.9 ni barabara ya LAMI, kilomita 154.43 ni barabara za Changalawe, na kilomita 568.6 ni barabara za udongo, kilomita 23.93 ni barabara zilizotengenezwa na kukarabatiwa pamoja na ujenzi wa madaraja matatu umekamilikwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 ikiwa ni matengenezo ya mara kwa mara. Aidha kwa mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya Tshs 800,000,000.00 zilitengwa kwa ajili wa ujenzi wa barabara za lami kilomita 1.5 ambapo mpaka Septemba 2019 jumla ya kilomita 1.114 zimetekelizwa na Wakandarasi wanaendelea na ukamilishaji. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya Tshs.6,552,571,498.00 zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza kilomita 12.2 za barabaraza za lami na kilomita 143.15 barabara za Changalawe.

Hali ya Wilaya ni ya milima na miinuko mikali na mabonde ambayo hupelekea barabara za Vijiji mara nyingi kutopitika hususani nyakati za masika. Kukosekana kwa matengenezo ya mara kwa mara kunasababishwa na ufinyu wa bajeti zinazotolewa kutoka mifuko mbalimbali. Athari ya hali hiyo inasababisha kushindwa kusafirisha mazao kwa wakati kutoka shambani hadi eneo la soko na hivyo kupelekea baadhi ya wakulima kupata hasara.

## **4.2 Simu**

Njia za mawasiliano Wilayani kama vile simu za kawaida, za upopo na simu za mkononi zinapatikana Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo ya Kiwira na Ushirika pia hata baadhi ya maeneo ya Vijijini. Hali hiyo inatokana na kupanuka kwa huduma zitolewazo na Taasisi mbalimbali kama kiwanda cha Chai, Hospitali za Mashirika ya Dini, Vituo vya Afya na Zahanati.

## **5. HUDUMA ZA KIFEDHA**

Mbali ya huduma za fedha kutolewa na SACCOS, Benki Kata pamoja na wakopeshaji binafsi hutoa pia huduma za kifedha. Wilaya inahudumiwa na Benki tatu za NMB, NBC na CRDB. Vyombo vingine vya kifedha ni BAY PORT. Vyombo vya PLATINUM, Blue Finance, Instant Credit na Faidika vinatoa huduma hasa kwa watumishi zikiwa na ofisi zao Mbeya mjini.

## **6. MAPATO YA HALMASHAURI**

Hadi kufikia Juni 2020, Halmashauri imekusanya jumla ya Tsh. **38,352,686,688.48** sawa na asilimia 81 ya makisio ya mwaka wa fedha 2019/2020 kama inavyoonesha hapo chini:-

### **Jedwali Na. 11: Mapato ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

<b>Chanzo cha mapato</b>	<b>Makisio ya mwaka 2019/2020</b>	<b>Kilichopokelewa Julai 2019– Juni, 2020</b>	<b>% ya mwaka</b>
Vyanzo vya Ndani	5,371,119,322.00	4,425,164,812.21	82
Ruzuku ya Mishahara (PE)	37,540,673,000.00	28,828,481,766.00	77
Mapato mengineyo, (OC)	1,371,976,100.00	830,760,599.67	61
Miradi ya maendeleo	3,320,109,079.25	4,268,279,510.60	129
<b>Jumla</b>	<b>47,578,212,303.5</b>	<b>38,352,686,688.48</b>	<b>81</b>

**Chanzo: Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuishia Juni 2020**

## **6.1 CHANGAMOTO ZA UKUSANYAJI WA MAPATO**

Changamoto zinazoikabili Wilaya kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani ni pamoja na; -

- a. Wananchi kukwepa kulipa ushuru na kodi za Halmashauri.

### **6.1.1 Mikakati ya uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato**

- i. Kubuni vyanzo vinya mapato ikiwa ni pamoja na ushuru wa magari, Ushuru wa mafuta ya mawese, Ushuru wa ada katika vyanzo vya utalii na Ushuru wa Minara ya simu.
- ii. Kupitia sheria ndogo za mapato ambazo ni za zamani na kuzibadilisha kulingana na wakati.
- iii. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kudhibiti mianya ya ukwepaji.
- iv. Matumizi ya mashine za kukusanya mapato (POS)
- v. Kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya umuhimu wa kulipa ushuru, ada na kodi.
- vi. Kushirikiana na wadau wengine kama Mahakama, Polisi na TRA katika ukusanyaji mapato.
- vii. Kuhamasisha wakulima wanaongeza uzalishaji wa mazao yao na kuwatafutia masoko ya mazao yao nje na ndani ya Wilaya.
- viii. Kuanzisha magilio ya Tarafa na Kata ili kudhibiti ununuzi wa mazao mashambani (uchumbiaji mashambani).

### **Changamoto za Halmashauri kwa ujumla**

1. Upungufu wa watumishi 846 kwa kada mbalimbali. Upungufu huu unatokana na kustaaifu, kufariki dunia; hasa katika idara za ujenzi, Afya, kilimo na mifugo.
2. Kuchelewa na kutofika fedha zote kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### **Utatuza wa changamoto**

1. Kibali cha kuajiri watumishi 846 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kimeombwa ili kuondoa upungufu huo imefanyika.
2. Kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutumia mashine za kukusanyishia mapato, kufanya doria za mara kwa mara kwa timu ya mapato ili kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa na kuimarisha uwezo wa Halmashauri kujitegemea.
3. Kuwa na vituo vya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa mazao yote yanayostahili kulipiwa ushuru yanalipiwa kabla hayajatoka nje ya Halmashauri.

**MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KWA HALMASHAURI YA RUNGWE**  
**YALIYOTOLEWA WAKATI WA ZIARA YA KIKAZI WILAYANI RUNGWE TAREHE 19/01/2018**

NA.	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI WA AGIZO	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
AGIZO NA. 1	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ifuatilie idhini ya ongezeko la fedha kiasi cha Sh. 263,806,980/- ya mradi wa Maji Masoko Skimu ya Mbaka kutoka Wizarani na Kamati ipate taarifa ya utekelezaji wa agizo hili kabla ya mwezi Mei 2018	Mhandisi wa Maji	Halmashauri iliomba kibali cha kuidhinishiwa kazi za nyongeza zenyenya thamani ya fedha kiasi cha Sh. 263, 806,980/- kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa barua Kumb Na.IMR/MSK/VOL.1/131/22 ya tarehe 12/02/2018. Wizara ilitoa idhini ya kuendelea na kazi hizo za nyongeza kwa barua yenye Kumb.Na.GC/279/547/01/B/51 ya tarehe 09/03/2018. Taarifa iliwasilishwa ofisi ya RAS kwa barua Kumb. Na. RDC/T.02/5Vol.III/ ya tarehe 03/05.2018. Aidha Mkandarasi hakuweza kuendelea na kazi kutokana na madai yake ya Tshs. 73,533,600/= kuchelewa kulipwa kwa zaidi ya miezi mitano kuanzia Mwezi February 2018 hadi Agosti 2018. Halmashauri imepokea fedha za mkandarasi kutoka Wizara ya maji tarehe 06/08/2018. Mkandarasi amerejea eneo la kazi baada ya kulipwa.	Agizo limetekelizwa			
AGIZO NA.2	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ifuatilie majibu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu tofauti ya Sh. 549,782,980 iliyongezeka wakati wa kufanya tathmini ya zabuni ya mradi wa Masoko skimu ya Bulongwe kwa barua Kumb.Na.RDC/PMU/F.1/VOL.II/164 ya tarehe 23/01/2018. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hajardhia tofauti ya gharama kiasi cha Sh. 549,782,980/- kilichotolewa na Kamati ya tathmini ya Zabuni ya mradi wa Masoko Skimu ya Bulongwe kwa barua ya siri Kumb.Na.AGCC/A/130/74/1 ya	Mhandisi wa Maji	Halmashauri imefuatilia majibu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu tofauti ya Sh. 549,782,980 iliyongezeka wakati wa kufanya tathmini ya zabuni ya mradi wa Masoko skimu ya Bulongwe kwa barua Kumb.Na.RDC/PMU/F.1/VOL.II/164 ya tarehe 23/01/2018. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hajardhia tofauti ya gharama kiasi cha Sh. 549,782,980/- kilichotolewa na Kamati ya tathmini ya Zabuni ya mradi wa Masoko Skimu ya Bulongwe kwa barua ya siri Kumb.Na.AGCC/A/130/74/1 ya	Agizo limetekelizwa			

NA.	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI WA AGIZO	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	ni sawa na 37% kama alivyoshauri kwenye mkataba na Kamati ipate taarifa ya utekelezaji wa agizo hili kabla ya mwezi Mei 2018.		tarehe 13/03/2018. Ameelekeza kuwa manunuzi yote yajayo taratibu za manunuzi zizingatiwe. Pamoja na maelekezo hayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa ushauri wa kuondoa jina la K.M.I.M. MSITA kama msuluhishi, ushauri ambao umezingatiwa kwa kufanya marekebisho ya mkataba husika. Pamoja na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Halmashauri kwa kushauriana na ofisi ya RAS imevunja mkataba huo kwa barua Kumb. Na.RDC/F2.B/139/23 ya tarehe 06/08/208. Hatua ya kuvunja mkataba imefikiwa kutokana na mkandarasi kushindwa kutekeleza mradi kwa majibu wa mkataba wake.				
AGIZO NA.3	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ihakikishe ifikapo tarehe 30 Aprili, 2018 mradi wa Maji Masoko uwe umekamilika kwa Mujibu wa Mkataba na taarifa ya utekelezaji wa mradi itumwe Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya na nakala kwa Ofisi ya Bunge kwa taarifa.	Mhandisi wa Maji	Kutokana na usimamizi na utekelezaji wa miradi ya Maji kuhamishiwa RUWASA kuanzia tarehe 1-07-2019 hii ikiwa ni pamoja na Mikataba na Mali nyinginezo za RUWASA ,Menejimenti ilipokea majibu ya utekelezaji wa agizo husika pamoja na majibu ya hoja za ukaguzi kupitia barua yenye Kumb Na. CA.3/71/02/08 ya tarehe 02-05-2020 na <b>Hali halisi ya utekelezaji miradi kufikia Aprili 2020 ni kama ifuatavyo:-</b> <ul style="list-style-type: none"> <li><b>Skimu ya Mbaka:</b> Mradi unatekelezwa na Mkandarasi M/S Mult Profession Co.LTD ambapo Gharama ya mradi ni Tsh 552,229,980 na fedha iliyolipwa ni Tsh 362,137,900 ambayo ni sawa na 65.6%. Utekelezaji wa mradi umefikia 95% na huduma ya maji inapatikana. Mkandarasi anamalizia</li> </ul>	Agizo linaendelea kutekelezwa	Tunashauri agizo ili lihamishiwe RUWASA ili kurahisisha ufuatiliaji.	Mali zote ikiwa ni pamoja na mikataba ya Miradi ya Maji imehamishiwa rasmi RUWASA kuanzia tarehe 01-07-2019 hivyo ni vema Agizo ili likamishiwa RUWASA	Maoni ya kamati ya fedha yafanyiwe kazi

NA.	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI WA AGIZO	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<p>kazi ndogo ndogo (snags) baada ya kulipwa fedha zake tshs. 60,000,000/= alizokuwa bado anadai na anatarajia kumaliza kazi hizo mwezi June 2020.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Skimu ya Ikama&amp;Itagata:</b> Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi Matrix Technolgy Co. LTD. Gharama za mradi ni Tshs 552,413,233 hadi sasa kiasi cha Tshs 272,633,309.60 kimeshalipwa ambacho ni sawa na 49.4%. Ujenzi unaendelea ambapo hadi sasa umeshafikia 70%. Hadi sasa vituo 30 vinatoa huduma ya maji kati ya vituo 67 vilivyojengwa. Utekelezaji unatarajija kukamilika tarehe 30 Juni 2020.</li> <li>• <b>Skimu ya Lufumbi&amp;Masoko:</b> Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi Msukwa Gen Enterprises, Gharama za Mradi ni Tshs 1,260,061,273.47 hadi sasa kiasi cha Tshs 1,015,767,291.11 kimeshalipwa ambayo ni sawa na 80.6%. Utekelezaji wa mradi umefikia 95% na huduma ya maji inapatikana katika Vijiji vya Lufumbi, Bujesi, Lupando, Lwifwa Busisya, Mbaka na Isabula Mkandarasi anamalizia kazi ndogo ndogo (snags) na mkandarasi anatarajia kumaliza mwezi Juni 2020</li> <li>• <b>Skimu ya Bulongwe:</b> Ujenzi wa skimu hii unatekelezwa kwa “Force Account” kwa</li> </ul>				

NA.	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI WA AGIZO	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<p>gharama ya shilingi 527,570,302.83 na kiasi kilichotumika ni tshs. 263,286,265.51 ni sawa na asilimia 50%. Hadi sasa utekelezaji wa shughuli za mradi umefikia asilimia 70%. Msimamizi mkuu wa mradi huu ni ofisi ya meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Skimu ya Kigange/Nsanga:</b></li> </ul> <p>Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi OSAKA STORES LTD na gharama ya mradi ni Tsh 851,625,619.00 hadi sasa kiasi cha Tsh 367,380,287.45 kimeshalipwa ambayo ni sawa na 43.14%. Utekelezaji wa mradi umefikia 80%. Hadi sasa vituo vyaya maji vyote 40 vinatoa huduma ya maji kwa wananchi wa Mpelangwasi na Nsanga. Mkandarasi anaendelea na kazi ya kukamilisha ujenzi wa chujio (treatment plant) la maji. Ujenzi wa chujio unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2020</p>				
AGIZO NA. 4	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe iweke mpango mpya wa kulinda Vyanzo vya Maji na miundombinu yote inayopitia katika Vijiji vyote vya mradi wa Maji Masoko kwa kuwashirikisha wananchi ili huduma hiyo ya maji wananchi	<b>Mhandisi wa Maji</b>	Halmashauri imeunda na kusajili Jumuia za Watumia Maji COWSO) katika Vijiji vyote 14 vitakavyonufaika na mradi ambazo zitahusika na kutunza na kulinda vyanzo vya maji na miundombinu yote ya mradi wa Maji Masoko katika Vijiji vyao.	<b>Agizo limetekelizwa</b>			

NA.	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI WA AGIZO	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	waweze kupata ili kuepuka uwezekano wa kutokea migogoro baina ya Wananchi.						
AGIZO NA.5	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ihakikishe inamaliza kazi ya mradi wa Maji Lugombo ndani ya muda wa Mkataba ili ifikapo tarehe 30 Machi 2018 kazi hiyo iwe imekamilika.	Mhandisi wa Maji	Kazi ya ujenzi wa mradi wa Maji Lugombo ilikamilika tarehe 12/02/2018 mwezi mmoja kabla ya muda wa mwisho wa mkataba wa mkandarasi. Mradi huo ulizinduliwa na mwenge tarehe 18/05/2018. Hadi sasa wananchi wa Lugombo wanaendelea kupata huduma ya maji.	Agizo limetekelizwa			
AGIZO NA.6	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ihakikishe mradi wa Maji Lugombo unawekewa uzio ili kuhakikisha usalama kwenye eneo la chanzo cha Maji, aidha Sheria ya matumizi ya vyanzo vya maji itumike ili shughuli za kibinadamu zisifanywe kuanzia umbali wa mita 60 kutoka chanzo cha maji.	Mhandisi wa Maji	Ujenzi wa uzio katika chanzo cha maji Ipanga tayari umekamilika na ulitekelezwa na Mkandarasi BERAS Inv Co. LTD kwa gharama ya Tshs 8,386,637.60  Aidha, shughuli za kilimo zilizokuwa zinafanyika ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji sasa zimesitishwa rasmi na eneo hilo kwa sasa limepandwa miti aina ya Mikuyu ambayo ni rafiki wa maji.	Agizo limetekelizwa			

**MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KWA HALMASHAURI YA RUNGWE**  
**YALIYOTOLEWA TAREHE 27/08/2018**

Na.	HOJA/ MAELEZO	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI	
1.	Utekelezaji wa Miradi ya Maji- Ucheleweshaji wa utekelezaji	Katibu Tawala Mkoa ameagizwa aunde Timu ya kufuatilia utekelezaji wa Miradi, Taarifa iandaliwe na kuwasilishwa NAO na kwa Katibu wa LAAC kabla au ifikapo tarehe 30/12/2018.	Mhandisi wa Maji	<p>Katibu Tawala Mkoa aliunda Timu ya wataalamu nane (8) tarehe 28/05/2018 kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maji Katika Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya ikiwemo Halmashauri ya Rungwe. Wataalamu walikamilisha kazi na kuwasilisha taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya mnamo tarehe 06/08/2018 na Halmashauri ya Rungwe Mnamo tarehe 24/08/2018 kwa barua Kumb. Na.CDE.63/283/01E/61 kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na timu hiyo.</p> <p>Katibu Tawala ameshawasilisha taarifa iliyotolewa na timu kwenye ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na Katibu wa Kamati ya LAAC.</p>	Agizo limetekelizwa				
2.	Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani	Mkurugenzi akiwezeshe kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa Rasilimali Fedha ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.	Mkaguzi wa Ndani	Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kitengo cha Ukaguzi kilitengewa bajeti ya Tshs 24,000,650 ambapo kiasi cha Tshs 20,000,000 ni fedha za mapato ya ndani na Tshs 4,000,650 ni ruzuku kutoka Serikali kuu.	Agizo limetekelizwa				

Na.	HOJA/ MAELEZO	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
				<p>Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kitengo cha ukaguzi wa ndani kimepangwi bajeti ya Tshs 34,000,650 ambapo Tshs 30,000,000 ni mapato ya ndani na Tshs 4,000,650 ni ruzuku kutoka serikali kuu. Pamoja na kutengwa kwa fedha hizi, kitengo cha Ukaguzi kimeendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufanikisha taarifa mbalimbali za ukaguzi, Menejimenti imeendelea kuzifanyia kazi kwa wakati taarifa za ukaguzi na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwa shughuli za halmashauri.</p> <p>Halmashauri itaendelea kukiwezesha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa rasilimali fedha na vifaa ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.</p>				
3.	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Madeni ya nyuma ya mfuko wa wanawake na Vijana.</li> </ul>	Halmashauri ioneshe mikakati ya kulipa madeni hayo na kuandika barua (Commitment Letter) kwa katibu wa kamati ya kudumu ya bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kabla ya Desemba, 2018.	DCDO/DT	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri imepokea barua yenyeye kumbukumbu namba CE.151/498/01/88 ya Tarehe 19-12-2019 ya ufutaji wa malimbikizo ya fedha za mikopo inayotokana na Asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri, kutokana na kufutwa kwa madeni ya</li> </ul>	Agizo limeteklezwa			

Na.	HOJA/ MAELEZO	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI	
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Madeni ya 20% ya vyanzo viliyofutwa kiasi cha Tsh 47,849,368</li> </ul>			<p>miaka ya nyuma kwa sasa Halmashauri haina madeni mapya</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri inalitambua deni hilo na hadi kufikia Machi,2020 imerejesha kiasi cha Tshs 12,359,400 kupitia Hati za Malipo Na 783042V1900512 ya 26/11/2018 na Hati ya Malipo Na 783042V1901848 ya 27/6/2019 na kiasi cha Tsh 35,489,968 kilichobaki, Halmashauri imepanga kurejesha kwa kwa miaka 2 ambapo kila mwaka itarejesha kiasi cha Tsh 17,744,984 kwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021</li> </ul>	<b>Agizo linaendelea kutekelezwa</b>	<b>Halmashauri iendelee kutekeleza mpango kazi wake wa urejeshaji fedha hizi</b>	<b>Menejimenti iendelee kupunguza deni kama mpango wa utekelezaji unavyoonesha.</b>	<b>Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe</b>	
4.	Utoaji wa Mikopo ya 10% kwa wanawake na Vijana	Halmashauri ifuate miongozo ya mfuko kwa kutoa mikopo hiyo kwa vikundi na sio kutuma SACCOS	DCDO	Halmashauri imetekeliza agizo ili kwa kuhakikisha inatoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemauvu na kuacha kupeleka fedha hizi katika SACCOS. Ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ilitoa kiasi cha Tshs 349,900,000 kwa vikundi Halmashauri ilitoa mikopo yenyenye jumla ya Tshs 349,900,000 kwa vikundi 63	<b>Agizo limetekeliza</b>				

Na.	HOJA/ MAELEZO	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI	
				vya wanawake (39) vijana (21) na walemavu (3)					
5.	Mapato ya Ndani	Halmashauri ishirikiane na Mkoa kupitia vyanzo vyote vya Mapato ili kuwa na uhakika wa kila chanzo ili bajeti ijayo ilingane na uhalisia wa makusanyo.	DPLO/DT	Halmashauri ilifanya tathimini ya kila chanzo kwa kupitia mapendekezo ya taarifa ya Tume ya kutathmini mapato kwa kila chanzo iliyoundwa na Katibu Tawala Mkoa. Maboresho yaliyofanywa na Halmashauri ni pamoja na kupitia sheria ndogo za ukusanyaji mapato kwa kila chanzo ambapo tayari rasimu ya awali ya maboresho ya sheria ndogo za ushuru na tozo mbalimbali za vyanzo vya mapato imeshawasilishwa kwenye vikao vya timu ya menejimenti pamoja na kamati ya fedha na uongozi.  Sambamba na hilo Halmashauri imepitia upya mikataba yake mbalimbali ikiwemo mikataba ya makampuni ya simu na kuiboresha ili kuhakikisha viwango vinavyolipwa vinaendana na wakati uliopo.  Maboresho yaliyofanyika yamezingatiwa wakati wa kuandaa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo Halmashauri imepanga	Agizo limeteklezwa				

Na.	HOJA/ MAELEZO	AGIZO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
				kukusanya kiasi cha Tshs 5,371,119,322 ikiwa Tshs 2,026,913,622 ni mapato fungiwa na Tsh 3,344,205,700 ni mapato halisi				
6.	'Retention Money' (Milioni 438)	Halmashauri ilipe deni la fedha hizo zilizotumika kwa shughuli zingine ili wakandarasi na wadai wengine waweze kulipwa. Kila malipo yanapofanyika vielelezo viwasilishwe Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAO). Deni hilo lilipwe ndani ya mwaka huu 2018/2019.	DT	Kiasi cha Tshs 215,700,441.80 kimeshalipwa kwa wakandarasi ambapo madai yao ni sehemu ya fedha zilizokuwepo kwenye Akaunti ya Amana wakati fedha hizo zilipokuwa zinakopwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maagizo mbalimbali.  Nyaraka za ulipwaji zimeambatanishwa. Halmashauri imeweka mkakati wa kumalizia deni hilo kama ifuatavyo: kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha Tshs. 111,460,110.58 na mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha Tshs. 111,460,110.58	<b>Agizo linaendelea kutekelezwa</b>	Halmashauri iendelee kutekeleza mpango kazi wake wa urejeshaji fedha hizi.	Menejimenti iendelee kupunguza deni kama mpango wa utekelezaji unavyoonesha.	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe
7.	Madeni ya Watumishi	Taarifa ya madeni ioneshe yote yakiwemo madeni yasiyo ya mishahara. Madeni hayo yaonekane kwenye kitabu cha LAAC na kitabu cha kufunga Hesabu za Mwaka husika.	DT	Halmashauri imetekeliza agizo husika kwa kuhakikisha taarifa za madeni yote yakiwemo madeni yasiyo ya mishahara yameingizwa kwenye kitabu cha LAAC na kitabu cha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni,2018	<b>Agizo limetekeliza</b>			

**MAJIBU YA UTEKELEZAJI WA HOJA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
2010/ 2011  2.2.16	Miradi isiyokamilika yenye thamani ya Tshs <b>1,075,655,000.</b>  i) Mradi wa maji wa Mwakaleli shs.1bl 'Intake'moja kati ya sita bado,vituo vya kuchochea maji(Domestic points)	Ushauri Na.1 Menejimenti ihakikishe miradi yote inakamilika kama ilivyopangwa na kuwe na usimamizi wa karibu ili kuongeza ufanisi	Kutokana na usimamizi na utekelezaji wa miradi ya Maji kuhamishiwa RUWASA kuanzia tarehe 1-07-2019 hii ikiwa ni pamoja na Mikataba na Mali nyinginezo za RUWASA ,Menejimenti ilipokea majibu ya utekelezaji wa hoja husika kuititia barua yenye Kumb Na. CA.3/71/02/08 ya tarehe 02-05- 2020 na hali halisi ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:- i) Awali mradi huu ulisimama kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha za utekelezaji, kutoka Wizara ya Maji. Kwa sasa ujenzi wa mradi wa maji Mwakaleli umefikia asilimia 60. Skimu 4 kati ya 6 zinatoa huduma ya maji ambazo ni  • <b>Mbaka:</b> Gharama ya ujenzi ni Tsh.683,452,489 na ujenzi umefikia asilimia 90 na huduma ya maji imeanza kupatikana	Eng Vicent Saronga-Meneja RUWASA  Wizara ya Maji  Miradi ya Maji inategemea Fedha kutoka Serikali Kuu, hivyo kuchelewa kukamilika kwake ilitokana na sababu ya kutoletwa au kuchelewa kuletwa fedha kutoka serikali kuu, hivyo hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na uzembe au hasara.	Hoja haijafungwa utekelezaji unaendelea	Tunashauri hoja hii ihamishiwe RUWASA ili kurahisisha ufuatliaji.	Mali zote ikiwa ni pamoja na mikataba ya Miradi ya Maji imehamishiwa rasmi RUWASA kuanzia tarehe 01-07-2019 hivyo ni vema hoja hii ikahamishiwa RUWASA	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiw e

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kigonya:</b> Gharama ya ujenzi ni Tsh. 1,036,083,848 na ujenzi umefikia asilimia 90 na huduma ya maji imeanza kupatikana</li> <li>• <b>Nswesi:</b> Gharama ya ujenzi ni Tsh. 277,953,590 na ujenzi umefikia asilimia 90 na huduma ya maji imeanza kupatikana.</li> <li>• <b>Mwakajwanga</b> Gharama ya ujenzi ni Tsh.166,342,853na ujenzi umefikia asilimia 90 na huduma ya maji imeanza kupatikana  Skimu 2 bado hazijakamilika ambazo ni;</li> <li>• <b>Suma</b> Gharama ya ujenzi ni Tsh. 1,154,889,069 na ujenzi umefikia asilimia 80. huduma ya maji inatarajiwa kuanza kupatikana mwezi Juni, 2020</li> <li>• <b>Ndala.</b></li> </ul>					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			Mradi huu umehamishiwa halmashauri ya wilaya ya Busokelo na Ujenzi wa skimu hii kwa sasa unatekelezwa kwa “Force Account” ambapo wasimamizi wake wakuu ni ofisi ya meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya.					
	(ii). Kiwanda cha Maziwa Katabe.	Ushauri 2 Menejimenti ihakikishe miradi yote inakamilika kama ilivyopangwa na kuwe na usimamizi wa karibu ili kuongeza ufanisi	(ii) Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa awamu mbili zimekamilika.  Ambapo jumla ya Tshs 126,000,000 zimetumika. Gharama ya mradi wote ni Tshs 1,047,343,856.9  Aidha, Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau Heifer International imeendelea na ukamilishaji wa Kiwanda ambapo ujenzi wa chumba kimoja, choo na mashimo ya maji taka umekamilika, pamoja na ununuzi wa tenki la lita 5,000 na jenereta kwa gharama ya Tshs 87,920,180/= na ukusanyaji wa maziwa umeanza	Dr. Lawrence Kibona-Afisa Mifugo na Uvubi  Miradi hii inatekelezwa kwa kupitia mapato ya ndani pamoja na wahisani, kutokana na Ukusanyaji wa mapato ya ndani kutofikia malengo ulichangia kutokamilika kwa mradi huu hivyo hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa.	Hoja haijafungwa, mradi unatekelezwa kwa awamu	Menejimenti iendelee kutenga bajeti ya mapato ya ndani pamoja na kuwashirikisha wadau wa maendeleo ili mradi husika uweze kukamilika	Menejimenti iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI	
			Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imetenga kiasi cha Tshs 20,000,000 kwa ajili ya kuendeleza mradi huu.						
2012/ 2013  2.3.14. 1	<b>Kutokarabatiwa kwa nyumba za watumishi wa Halmashauri</b> Halmashauri inatakiwa kutoa mazingira wezeshi, rafiki na salama kwa watumishi wa Halmashauri. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imeonekana kuwa nyumba za watumishi zimechakaa na hazijafanyiwa ukarabati na hakuna mpango wa ukarabati.	<b>Ushauri Na.3</b> Menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuwa na sera na mipango ya ukarabati wa nyumba za watumishi na imekuwa ikifanyika kwa awamu: 2011/2012 ulifanyika ukarabati wa nyumba za watumishi uliogharimu kiasi cha Tsh 17,000,000.00,  Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 nyumba ya makazi ya Mkurugenzi na Afisa rasilimali watu wa Wilaya zilikarabatiwa kwa kiasi cha Tsh Tshs 26,000,000.00.  Kwa mwaka 2017/2018, jumla ya nyumba 7 za watumishi wa makao makuu ya Halmashauri zilikarabatiwa kwa jumla ya Tshs. 115, 000,000.00 na nyumba 15 za walimu wa shule ya msingi kwa Tshs. 45, 000,000.00 na kwa mwaka 2019/2020 imetengwa bajeti ya Tshs 50,000,000.00 kwa ajili ya	Kumekuwa na mipango ya ukarabati wa nyumba za watumishi na imekuwa ikifanyika kwa awamu: 2011/2012 ulifanyika ukarabati wa nyumba za watumishi uliogharimu kiasi cha Tsh 17,000,000.00,  Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 nyumba ya makazi ya Mkurugenzi na Afisa rasilimali watu wa Wilaya zilikarabatiwa kwa kiasi cha Tsh Tshs 26,000,000.00.  Kwa mwaka 2017/2018, jumla ya nyumba 7 za watumishi wa makao makuu ya Halmashauri zilikarabatiwa kwa jumla ya Tshs. 115, 000,000.00 na nyumba 15 za walimu wa shule ya msingi kwa Tshs. 45, 000,000.00 na kwa mwaka 2019/2020 imetengwa bajeti ya Tshs 50,000,000.00 kwa ajili ya	<b>Husna Toni-Afisa Mipango</b> <b>Anyonisy Mwasege- Mhandisi wa Ujenzi</b>	<b>Hoja haijafungwa utekelezaji unaendelea</b>	<b>Menejimenti iendelee kuongeza ukusanyaji wa mapato ili iweze kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za watumishi</b>	<b>Menejimenti iendelee kuongeza ukusanyaji wa mapato ili iweze kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za watumishi</b>	<b>Menejimenti iendelee kuongeza ukusanyaji wa mapato ili iweze kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za watumishi</b>	<b>Maoni ya kamati ya fedha yazingatiw e</b>

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			ukarabati wa nyumba 5 za watumishi. Ambapo ukarabati umeshaanza kwa nyumba zilizopangwa. Serikali Kuu imeongeza kiasi cha sh. 50,000,000.00 kwa mwaka 2019/2020 kukamilisha nyumba 2 za watumishi katika shule za Msingi Isuga na Lufingo ambapo ujenzi wake unaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imetenga kiasi cha sh. 40,000,000.00 kukarabati nyumba 5 za watumishi.					
2013/ 2014  3.8.3	Miradi isiyokamilika yenye thamani ya TSh.342,400,000  Wakati Timu ya ukaguzi ilipotembelea Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe tarehe 04 hadi 06 Septemba 2014, ilionekana kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilitekeleza miradi yenye thamani ya Tsh .342,400,000 chini ya Mfuko wa kukuza mitaji wa Mamlaka ya Serikali za	Ushauri Na 4 Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuhamkisha utekelezaji wa miradi, ufuatilaji na tathmini ya miradi hiyo inafanyika katika muda uliopangwa. Pia, Halmashauri inashauriwa kuhamasisha Jamii kuwa na ushiriki	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi, Mapendekezo ya Mkaguzi yameendelea kufanyiwa kazi. Fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya kusaidia ukamilishaji ambapo utekelezaji unafanyika kwa kushirikiana na wananchi. Kiasi cha fedha kilichotolewa kimetumika na Baadhi ya miradi yenye thamani ya shilingi 252,000,000.00 imekamilika na inatumika. Miradi hii inajumuisha:- -Nyumba ya mwalimu (S/Msingi Busona)	Husna Toni-Afisa Mipango  Wizara ya Fedha  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya watumishi kwa sababu tatizo hili linatokana na ukosefu na kutoletha kwa fedha kwa wakati.	Hoja haijafungwa, kwa kuwa baadhi ya miradi bado haijakamilika	Halmashauri iweke kipaumbele kwenye ukamilishaji wa miradi ya zamani kabla ya utekelezaji wa miradi mipya	Menejimenti iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	Mitaa (LGCDG)  Hata hivyo, miradi hii haikuwa imekamilika hadi wakati wa ukaguzi.	kamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.	- Nyumba ya mwalimu (Shule ya Sekondari Ukukwe). - Jengo la Ofisi ya Kata ya Matwebe - Nyumba ya mwalimu (Shule ya Sekondari Kisiba). - Nyumba ya mwalimu (S/Msingi Bunyangomale) - Nyumba ya mwalimu (S/Msingi Kibwe) -Jengo la Ofisi ya Kata ya Kyimo - Jengo la Ofisi ya Kata ya Itagata - Nyumba ya mwalimu (S/Msingi Mpelangwasi) - Nyumba ya mwalimu ( S/Msingi Lubemba) - Nyumba ya mwalimu (S/Msingi Bunyakasege)  Aidha, miradi yenyeye thamani ya Tshs.90,400,000 utekelezaji wake unaendelea kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau wa maendeleo. Uongozi wa Halmashauri umeshatoa hamasa kwa Jamii kushiriki katika umaliziaji wa miradi ambayo haijakamilika kwa kuchangia fedha na vifaa hitajika ambapo					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 kiasi cha sh. 80,000,000.00 kimetengwa kutoka mapato ya ndani ili kusaidia jitihada za jamii kukamilisha miradi mbalimbali. Miradi ambayo bado ujenzi wake haujakamiliika ni ukamilishaji wa Ofisi za Kata Masukulu, Bagamoyo na Ibigi. Halmashauri itaendelea kupanga bajeti kwa mwaka 2021/2022 ili kukamilisha miradi.					
2014/2015 3.16.1	<b>20% ya fedha kutorejeshwa na Halmashauri Vijijini. Tshs. 545,840,695/=</b> Wakati wa ukaguzi, jumla ya Tshs. 107, 393,000 zilipokelewa kutoka Serikalini kama fedha za fidia ya vyanzo vilivyo futwa, Tshs. 3,015,296,405/= zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri na kufanya jumla ya Tshs. 3,122,689,405/. Ukaguzi umebaini kwamba Tshs.	Ushauri Na.5 Menejimenti ihakikishe kiasi cha Tshs. 545,840,695/= kinapelekwa Vijijini kama inavyotakiwa.	Menejimenti inayatambua madeni hayo 20% ya Vijiji. Aidha Halmashauri imepanga kuhakikisha madeni yote yanalipwa kwa mkakati ufuatao; - 2019/20 Shs.61,450,000/= 2020/21 Shs.73,880,000/= 2021/22 Shs.71,890,000/= 2022/23 Shs.65,750,000/= 2023/24 Shs.66,955,000/= 2024/25 Shs.68,000,695/= 2025/26 Shs.68,895,000/= na 2026/27 Shs.69,020,000/=  Aidha Kwa sasa Halmashauri inaendelea kutimiza matakwa ya kisheria kwa kuhakikisha 20% zinapelekwa kwenye ngazi za	Lucas Ndombele-Mweka Hazina  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa sababu hoja hii imetokana na Ukusanyaji wa mapato ya ndani kutofikia malengo	Hoja haijafungwa	Halmashauri iendelee kutekeleza mpango kazi wake wa urejeshaji fedha hizi.	Menejimenti iendelee kutekeleza mpango kazi wa urejeshaji	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	78,697,186/= tu ndizo zilizopelekwa vijiji badala ya Tshs 624,537,881/= na kuacha Tshs 545,840,695/= sawa na asilimia 87.4.		Vijiji kama ilivyopangwa. Ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imepeleka kiasi cha Shs.179,085,720 na kwa mwaka 2017/2018 Halmashauri imepeleka kiasi cha Tshs.290,614,050.00 na kwa mwaka wa fedha 2018/2019 mpaka mwezi Mei mwishoni Halmashauri imepeleka kiasi cha Sh.339,397,353.8					
2014/2015 3.21.1	<b>Kutokamilika kwa Miradi ya Maendeleo yenye thamani ya Tshs 2,395,825,326/=</b>  <b>Kilimo</b> Matengenezo ya miundo mbinu ya barabara Matwebe – Mpakani Tshs 43,949,405.50 Matengenezo ya miundo mbinu ya barabara kijiji cha Isuba Tshs 70,310,090.50 Ujenzi wa kituo cha rasilimali kilimo kijiji cha llenge Tshs 35,000,000 Matengenezo ya barabara kijiji cha Isuba na Mpakani Tshs 87,919,527	Ushauri Na. 6 Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuwasiliana na Wizara husika ili fedha ziletwe ili kukamilisha miradi hiyo.	<b>Kilimo</b> Miradi yote ya kilimo iliyohojwa imekamilika na inatumika.  <b>Maji</b> Utekelezaji wa Miradi ya Maji;- Mradi wa Maji Syukula; Mradi umekamilika na unatoa huduma kama iliyokusudiwa.  Mradi wa Maji Itete na Kapugi; Mradi huu umekamilika na unatoa huduma kama ilivyopangwa.  <b>Mradi wa Maji Isyonje;</b> Utekelezaji wa mradi wa maji Isyonje umekamilika na huduma ya maji inapatikana	<b>Wizara ya Fedha</b> Miradi hii imechelawa kukamilika sababu ya Kutoletwa/ kuchelewa kuletwa fedha kutoka serikali kuu pamoja na Ukusanyaji wa mapato ya ndani kutofikia malengo hivyo hakuna uzembe au hasara iliyosababishwa na watumishi	<b>Hoja imefungwa</b>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p><b>MAJI</b>  Ujenzi wa mradi wa maji  Syukula Tshs 397,313,737  Ujenzi wa Mradi wa maji Itete  na Kapugi Tshs 289,127,930  Mradi wa maji Isyonje Tshs  100,980,000.  Mradi wa maji Kijiji cha Ijigha na  Masukulu Tshs 263,461,581.26  Mradi wa maji Nkunga Tshs  104,090,000.  Mradi wa maji Kijiji cha Katabe  Tshs 106,986,652.  Mradi wa maji Lugombo Tshs  30,775,000.  Mradi wa maji Ilolo Tshs  80,999,100.</p> <p><b>LGCDG</b>  Matengenezo ya Ofisi ya Kata  Kisondela Tshs 10,000,000.  Ukarabati wa Zahanati ya  Ntokela Kata ya Isongole Tshs  1,000,000 na Kituo cha Afya  Masukulu Tshs 1,867,506.</p> <p><b>BARABARA</b>  Matengenezo ya barabara ya  lami Tukuyu Mjini Tshs  110,524,047.32</p>		<p><b>Mradi wa Maji Kijiji cha Ijigha  na Masukulu;</b>  Mradi umekamilika na unatoa  huduma kama ilivyopangwa.</p> <p><b>Mradi wa maji Nkunga;</b>  Mradi umekamilika na unatoa  huduma kama ilivyopangwa</p> <p><b>Mradi wa maji Ilolo;</b>  Mradi umekamilika na huduma ya  maji inapatikana</p> <p><b>Miradi ya LCDG;</b>  Miradi yote imekamilika na  inatumika.</p> <p><b>Barabara:</b>  Matengenezo ya barabara ya  Lami Tukuyu Mjini ya thamani ya  Tshs. 110,524,047.32  yamekamilika na barabara  inatumika.</p>					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
2015/ 2016 2.18.1	Miradi isiyokamilika yenye thamani ya TZS 25,500,000 Wakati wa kutembelea miradi ya maendeleo uliofanyika tarehe 29 hadi 30 Oktoba 2016, iligundulika kuwa baadhi ya miradi haikuwa imekamilika kwa wakati.	Ushauri Na. 7  Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati na kwa gharama halisi (realistic estimations).	Kiasi cha Sh. 25,500,000/- kilipangwa kusaidia kutekeleza miradi 11 ambapo kiasi chote kilichotolewa kilitumika.  Miradi 7 yenye thamani ya sh 15,500,000.00 imekamilika na inatumika.  Miradi hiyo ni ukarabati wa darasa S/M Makandana, ujenzi wa matundu ya vyoo Sm Lupale, Mpumbuli, Ibighi na Lufingo, kukarabati darasa sm Lukingi, na umaliziaji wa darasa Sekondari ya Kalengo  Aidha mradi 1 uliyobaki yenye thamani ya Tsh 10,000,000.00 kiasi cha Tsh. 10,000,000.00 kimetengwa katika bajeti ya 2020/2021 kukamilisha jengo la Utawala Sekondari ya Ilima.	Husna Toni-Afisa Mipango  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya watumishi kwa sababu kutokea kwa hoja hii ni kutokana na kuchelewa kuletwa kwa fedha kutoka Hazina na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji.	Hoja haijafungwa kwa kuwa utekelezaji unaendelea	Halmashauri iweke kipaumbele kwenye ukamilishaji wa miradi ya zamani kabla ya utekelezaji wa miradi mipya	Menejimenti iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe
2016/1 7 2.10.2	Kutokamilika kwa miradi mbalimbali ya CDG kiasi cha Sh. 33,085,800.00  Katika ukaguzi wa mwaka ilibainika kuwa miradi ya CDG ilitoa fedha kiasi cha sh.	Ushauri Na. 8  Menejimenti inashauriwa kuhakikisha miradi inayoibuliwa inakamilika kwa	Halmashauri kwa mwaka 2016/2017 ilipokea kiasi cha sh. 275,075,200.00 kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali. Miradi yote iliyopata fedha kuitia fedha za CDG ikiwemo iliyohojiwa imekamilika:	Husna Toni-Afisa Mipango  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi	Hoja haijafungwa, aidha utekelezaji unaendelea	Halmashauri iweke kipaumbele kwenye ukamilishaji wa miradi ya zamani kabla ya	Menejimenti iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	33,085,800.00 kukamilisha miradi ya ujezi wa vyumba nya madarasa, vyoo na nyumba za walimu katika shule za msingi na sekondari katika Halmashauri	wakati, pia kuhakikisha jamii inahamasishwa kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.	- Madarasa 3 S/m Lubemba (6,000,000) - Madarasa 2 S/m Ibuka (5,000,000) - Nyumba2 za walimu S/m Kituli(4,000,000) - Darasa 1 S/m Iponjola (4,000,000) - Darasa 1 S/m Malangali (3,000,000) - Nyumba 3 za walimu S/m Itiki (8,000,000) - Nyumba 1 ya Mwalimu S/m Ikomelo (4,000,000)	ya watumishi kwa sababu hoja hii ilitokana na ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa shughuli za miradi hii.		utekelezaji wa miradi mipya		
2016/2017 2.11.3	20% ya Fedha za fidia ya vyanzo vilivyo futwa kutorejeshwa Vijini Shs 47,849,368. Wakati wa ukaguzi jumla ya Tshs.47,849,368= za fidia ya vyanzo vilivyo futwa kwa muda wa miaka mitatu hazikupelekwa vijiji kama ifuatavyo; <ul style="list-style-type: none"><li>• Mwaka 2014/15 Shs 26,314,368.</li><li>• Mwaka 2015/16 Shs</li></ul>	Ushauri Na.9  Mnejimenti ihakikishe kiasi cha Tshs. 47,849,368/= kinapelekwa Vijiji kama inayotakiwa.	Halmashauri inalitambua deni hilo na hivyo imejipanga kulirejesha kwa mpango ufuatao:- kwa mwaka 2018/2019 itarejesha Tsh.16,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2019/2020 itarejesha Tsh.18,000,000/= na kwa mwaka 2020/2021 itarejesha Tsh.13,849,368/= Hadi kufikia robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2019/2020 tayari Halmashauri imerejesha kiasi cha Tshs 12,359,400 kupitia Hati za Malipo Na 783042V1900512 ya 26/11/2018	Lucas Ndombele-Mweka Hazina  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na hoja hii kutokuwa na uzembe au ubadhirifu wa fedha, Halmashauri imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa	Hoja haijafungwa, aidha utekelezaji unaendelea	Halmashauri iendelee kutekeleza mpango kazi wake wa urejeshaji fedha hizi	Mnejimenti iendelee na utekelezaji wa mpango kazi wa urejeshaji	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	4,694,400. • Mwaka 2016/17 Shs 16,840,600		na Hati ya Malipo Na 783042V1901848 ya 27/6/2019 Halmashauri itaendelea kupeleka kiasi kilichosalia kulingana na upatikanaji wa mapato ya ndani.	vijjini kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2020/2021				
2016/ 2017 2.11.4	Fedha zilizokopwa kutoka kwenye akaunti ya amana ambazo hajizarejeshwa kiasi cha Tshs. 438,620,663	Ushauri Na.10  Uongozi wa Halmashauri unashauriwa yafuatayo  <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuhakikisha fedha zote zilizokopwa zinarejeshwa na vielelezo viwasilishwe kwa mkaguzi kwa ajili ya uhakiki</li> <li>• Kuimarisha udhibiti wa ndani kwenye akaunti ya amana.</li> </ul>	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi, Hoja hii ni ya kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015, Fedha hizi zilizimwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo:-  <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kujenga maabara kwa agizo la Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.</li> <li>• Kutengeneza madawati kwa shule za Msingi na Sekondari.</li> <li>• Kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Desemba 2014 Maombi haya yaliruhusiwa na vikao vya kamati ya fedha utawala ana mipango viliviyoketi tarehe 20/11/2014 na 24/03/2014 kuititia DO.NA.FUM. 558/05/2014/2015 DO.NA.FUM.600/09/2014/2015.</li> </ul>	Lucas Ndombele-Mweka Hazina  Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na hoja hii kutokuwa na uzembe au ubadhirifu wa fedha, hata hivyo fedha zimeagizwa na kamati ya bunge ya hesabu za serikali za mitaa ziwe zimerejeshwa zote hadi kufikia juni,2019	Hoja haijafungwa, aidha utekelezaji unaendelea	Halmashauri iendelee kutekeleza mpango kazi wake wa urejeshaji fedha hizi.	Mnejimenti iendelee na utekelezaji wa mpango kazi wa urejeshaji	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<p>Sehemu ya fedha hizi zilikopwa ilikuwa ni fedha za wakandarasi (Retention money), aidha Katika kupunguza madeni yaliyotokana na fedha hizi kukopwa, Kiasi cha Tshs 15,000,000 killipwa kwa TARURA mwezi Januari, 2018 ili kuwalipa wakandarasi wanaodai.</p> <p>Vilevile Halmashauri imeshalipa kiasi cha Tshs 200,700,441.84 kwa wakandarasi wa maji, LUKOLO CO. LTD Kiasi cha Tsh 144,655,393.52 kwa PV Namba 783042V1900604 Kiasi cha Tsh 20,196,554 kimelipwa kwa NGOGO ENGINEERING CO.LTD kwa PV Na.783042V1900760 pamoja na M/S. INTERCOUNTRY ROAD CONSTRUCTION CO.LTD. kiasi cha Ts 35,848,494.32</p> <p>Viambata vyta ulipwaji wa madeni hayo vimewasilishwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa ajili ya uhakiki.Hata hivyo Halmashauri imeweka mkakati wa kumalizia deni hilo kama ifuatavyo: 2019/2020 Tshs.</p>					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			111,460,110.58 na mwaka wa fedha 2020/2021 Tshs. 111,460,110.58					
2017/1 8 2.4.1	<b>Utunzaji wa Mali za Kudumu</b>  <b>Uwepo wa magari sita (6) na pikipiki (7) mbovu ambazo hazitumiki.</b>  Wakati wa ukaguzi, tulibaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina magari sita (6) na pikipiki saba (7) ambazo zimetelekezwa muda mrefu pasipo kutengenezwa au kuuzwa kinyume na kifungu Na. 45 (1)-(3) cha Mwongozo wa usimamizi wa Fedha za Serikali za Mitaa za mwaka 2009 ambacho kinaeleza kwamba mali zote ambazo hazitumiki, zilizokwisha muda wa matumizi, mbovu/au zisizoweza kutengenezwa	Ushauri Na. 11 Menejimenti inashauriwa kuhakikisha kwamba mali zote zipo salama na zile mbovu ambazo hazitumiki zinapaswa kutengenezwa au kuuzwa/kufutwa ili kuepuka usababishaji wa hasara wa mali za Serikali	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi Magari yenyе Nambari SM 4704, STJ 7887 na SM 11426 yanaendelea kufanyiwa matengenezo katika hatua mbalimbali za matengenezo. Sambamba na hilo, magari yenyе nambari SM 85, STH 1130, SM 1301 na STG 9983 na pikipiki yenyе nambari STG 3167 yalishafanyiwa uhakiki na Bodи ya Uhakiki Mali (Board of survey) kupitia ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali na kuombewa kibali cha kuuza magari hayo kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha kupitia barua yenyе kumb. Na. SVR/MBR/KUMM/23/Vol.IX/20 ya tarehe 13.02.2020. Aidha, pikipiki zingine sita (6) zilishafanyiwa matengenezo na zinatumika katika shughuli	<b>Mhandisi- Anosisye Mwasege</b>  <b>Victor Mwakapala- Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi</b>  Hakuna hatua iliyochukuliwa kwa Watumishi hawa kwa kuwa tayari utekelezaji wa hoja hii unaendelea kufanyika.	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	zinapaswa kutambuliwa na kufutwa/kuuzwa baada ya kuridhiwa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na hatimaye Baraza la Madiwani.		mbalimbali za kiofisi.					
2017/18 2.6.1	<b>Mapitio ya Bajeti</b> <b>Kutolewa kwa fedha pungufu za bajeti ya Shughuli za Mazingira TZS 380,500,000</b> Wakati wa mapitio ya bajeti ya mwaka husika, Halmashauri ilipanga bajeti ya TZS 400,750,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mazingira. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30/6/2018 Halmashauri ilitoa kiasi cha TZS 20,250,000 kutoka kwenye bajeti iliyopangwa hivyo kusababisha upungufu wa TZS 380,500,000 ambao ni sawa na 93 % ya fedha za bajeti za mazingira	Ushauri Na.12 Tunashauri uongozi wa Halmashauri kupitia shughuli ambazo hazikutekelezwa kwa kuzipangia tena bajeti kwenye mwaka ujao wa fedha kwa kuangalia vipaumbele vya shughuli husika	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi, idara ya usafi na mazingira imepitia upya shughuli ambazo hazikutekelezeka kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutokana na ufinyu wa bajeti kwa kuangalia vipaumbele katika kutekeleza majukumu yake ambapo shughuli hizo zilitekelezwa kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 kama ifuatavyo: i)Ununuzi wa vifaa kinga-Tshs 300,000.00- ununuzi haujafanyika vifaa vya kufanya kazi vimepatikana kutoka kwa mdau (METL) ii)Uandaji wa taarifa za mazingira-Tshs 300,000.00 - fedha imetolewa na taarifa zimeandaliwa na	<b>Salum Kilanga-Afisa Mazingira</b> Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kwa sababu hoja hii ilichangiwa na ufinyu wa mapato ya ndani hivyo kushindwa kutekelezwa kwa shughuli zilizopangwa.	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<p>kuwasilishwa mamlaka husika</p> <p>iii)Uhamasishaji wa usafi wa mazingira-Tshs 5,000,000 – uhamasishaji umefanyika kata 29</p> <p>iv)Ufutiliaji wa utekelezaji wa sheria ya mazingira kwa Halmashauri nzima-Tshs 2,000,000- ufutiliaji umefanyika Aidha badala ya ununuzi wa gari la Taka ambalo lingegharimu kiasi cha Tshs 150,000,000 Halmashauri imefanya matengenezo ya magari yake mawili SM 4060 pamoja na SM 4704 ya kubebeta taka kwa gharama ya Tshs 23,000,000 hivyo kurahisisha shughuli za uzoaji wa taka.</p>					
2017/1 8 2.8.2	<b>Mapungufu katika utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani</b> Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sehemu ya 45(1) ya mwaka 1982 na marekebisho ya 2000 pamoja na Kifungu 14(4) cha Mwongozo wa Fedha	<b>Ushauri Na.13</b> Tunashauri Halmashauri kwa kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha inafanya kazi mapungufu	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi, mapungufu yaliyobainishwa yameendelea kufanyiwa kazi na uongozi ambapo: i. Uongozi umeendelea kuwasiliana na mamlaka	<b>Simon Mutabazi-Kaimu Mkaguzi wa Ndani</b> Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa hoja husika imetokana	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2009 kinalekeza Afisa Masuuli kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani wakati wa ukaguzi mapungufu mbalimbali yalibainika</p> <p>i)Mkuu wa kitengo alikua bado ana kaimu kwa zaidi ya miezi 11</p> <p>ii)kuna upungufu wa watumishi 3 ambapo wanatakiwa watumishi 5 ila wapo 2</p> <p>iii)Ukaguzi ulibaini kitengo kimepangiwa bajeti ya Tsh 10,000,000 kupitia mapato ya ndani na Tsh 5,980,000 kutoka ruzuku ya Serikali Kuu, ambapo kitengo kilipokea kiasi cha TZS 300,000 kutoka mapato ya ndani na TZS 1,955,000 kutoka ruzuku ya serikali kuu ambayo ni sawa na 14% ambayo inaonesha hakuna uwezeshaji kwa kitengo kuweza kutekeleza majukumu yake</p> <p>iv)Wakaguzi waliopo walikuwa hawajapatiwa mafunzo ya mifumo mbalimbali ambayo inatumika katika Halmashauri kama LAWSON, FFARS</p>	mbalimbali yaliyobainika	<p>husika kwa ajili kuthibitishwa kwa ya watumishi wanaokaimu katika nafasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mkaguzi wa ndani.</p> <p>ii. Moja ya agizo la LAAC, Halmashauri ilielekezwa kuhakikisha kitengo cha ukaguzi kinamarishwa kwa kupewa vitendea kazi pamoja na fedha za kutekeleza kikamilifu majukumu yake mbalimbali Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kitengo cha Ukaguzi kilitengewa bajeti ya Tshs 24,000,650 ambapo kiasi cha Tshs 20,000,000 ni fedha za mapato ya ndani na Tshs 4,000,650 ni ruzuku kutoka Serikali kuu.Ambapo kitengo kilipokea jumla ya Tshs 13,430,728</p> <p>Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kitengo cha ukaguzi wa ndani kimepangiwa bajeti ya Tshs 34,000,650 ambapo Tshs 30,000,000 ni mapato ya ndani</p>	na ufinyu wa bajeti.				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	(Financial Facility Accounting and Reporting System), POS, PLANREP and GoT HOMIS v)Kitengo kina upungufuwa viendea kazi ikiwemo kompyuta mpakato vi)Kitengo kina andaa mpango kazi wake lakini utekelezaji wake ulikuwa haujamilika kama kukosekana kwa taarifa za mfuko wa Afya, miradi ya maji, Barabara huku taarifa za TASAF zikiwepo vii)Kasi ndogo ya utekelezaji hoja za Mkaguzi wa ndani viii)Kutoandaliwa kwa taarifa ya mwaka ya ukaguzi kama Kifungu Na. 14 (7)(b) cha LGFM, 2009 kinavyoelekeza ix) Kutouwepo kwa Working papers kama inavyoelekezwa na Kifungu Na. 14(5) cha LGFM, 2009.		na Tshs 4,000,650 ni ruzuku kutoka serikali kuu. Hadi kufikia 30 Machi,2020 Kitengo cha Ukaguzi kimeshapeka kiasi cha Tsh 6,014,451.97 vilevile imepokea kiasi cha Tshs 1,516,000 kama ruzuku kutoka serikali kuu. iii. Halmashauri itaendelea kuhakikisha wakaguzi wanapatiwa mafunzo mbalimbali kulingana na upataikanaji wa fedha ambapo kiasi cha Tsh 4,000,000 kimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwa wakaguzi iv. Halmashuri itahakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. v. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kitengo cha ukaguzi wa ndani kimekagua miradi mbalimbali inayotekelizwa katika Halmashauri ikiwemo miradi ya ujenzi na ukarabatiwa kituo cha Afya, miradi ya Maji. Miradi ya barabara					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
			<p>haipo kwenye mpango kazi wa kitengo cha Ukaguzi baada ya shughuli zake kuhamishiwa TARURA, Taarifa za Ukaguzi zipo tayari kwa ajili ya uhakiki.</p> <p>vi. Uongozi umeendelea kusisitiza kufanyiwa kazi kwa hoja za Mkaguzi wa Ndani kwa wakati, kwani hoja hizo ambazo hazifanyiwi kazi ndizo zimekuwa zikijitokeza kwenye Taarifa ya Mkaguzi wa Nje.</p> <p>vii. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kitengo cha Ukaguzi kitaandaa taarifa ya mwaka ya ukaguzi kama matakwa ya kifungu Na. 14(5) cha LGFM, 2009 kinavyoelekeza.</p> <p>viii. Kitengo cha ukaguzi kinaanda working papers na kuweka kwenye jalada husika kama inavyotakiwa na zipo tayari kwa ajili ya uhakiki.</p>					
2017/18	Mfumo wa Taarifa za kiutumishi na Mishahara	Ushauri Na.14	Tunakubaliana na mapendekezo ya Mkaguzi. Uongozi wa	Jumanne Chaula-DHRO	Hoja hajafungwa	Halmashauri iendelee	Menejimenti iwasiliane na	Maoni ya kamati ya

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
2.10 2.10.1	(HCMIS)  Mfumo wa Taarifa za kiutumishi na Mishahara umetengenezwa na unaruhusu Maafisa Utumishi kuhifadhi na kurekebisha taarifa za watumishi kupitia mfumo wa "Lawson toleo la 9" ambapo mfumo huu unatoa nafasi ya kufanya marekebisho yote ya lazima. Serikali ya Tanzania hutumia mfumo huu kwenye Wizara mbalimbali, idara mbalimbali, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wakati wa ukaguzi, wakaguzi walitaka kuona tija ya mfumo huu na jinsi unavyotumika ambapo walibaini mapungufu yafuatayo katika utumiaji. i)Mfumo una matumizi 6 tofauti tofauti (Rasilimali watu- HR, Taarifa za Watumishi-PA, na Taarifa za mishahara – PR, General ledger-GL, Stahiki-BN and wasiokuwepo-LP) lakini ni njia moja tu ambayo hutumika na Halmashauri ambayo ni Rasilimali watu- HR	Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kufanya juhudhi za makusudi za kuongeza utendaji kazi wa kitengo cha Habari na Mawasiliano ya Kompyuta na kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili waweze kurekebisha mapungufu ya mfumo yaliyobainika.	Halmashauri unafahamu mapungufu ya mfumo yaliyobainishwa na Mkaguzi na yatawasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili waweze kurekebisha mapungufu ya mfumo yaliyobainika.	Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kwa mapungufu yaliyopo kwenye mfumo wa Lawson 9; yanapaswa kurekebisha na Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma.		kuwasiliana na mamlaka husika ili mapungufu yaliyobainishwa katika mfumo yafanyiwe kazi	mamlaka husika ili kutatua changamoto zilizobainishwa	fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIWA A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>ii)Mfumo wa Lawson hauna uwezo wa kutambua watumishi watoro ili wachukuliwe hatua za kinidhamu.</p> <p>iii)Mfumo wa Lawson hauna uwezo wa kutambua watumishi ambao wamechukua likizo ya mwaka, likizo ya ugonjwa, likizo bila malipo, likizo ya uzazi, likizo ya kustaafu nyingine.</p> <p>iv)Mfumo wa Lawson kuonesha utendaji kwa kuangalia msingi ukilinganisha na utendaji wa sasa na upimaji wa wazi (OPRAS) na mamlaka ya waajiri wote kwenye marekebisho ya sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007. Lakini misingi hii haifanyiwi kazi.</p> <p>v)Mfumo wa Lawson hauwezi kutambua moja kwa moja kuwa Mtumishi amechukuliwa hatua za kinidhamu, amepunguzwa kazini, ameshushwa cheo na aliyefukuzwa kazi.</p> <p>vi)Mfumo wa Lawson hauwezi kupima utendaji wa watumishi kwa kulinganisha elimu walijonayo, aina ya mafunzo</p>	Halmashauri.						

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIWA KWA WAHUSIKA WALIOSABABISHA A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>yanayohitajika ili kufikia kiwango kinachohitajika kiutendaji.</p> <p>vii) Taarifa za watumishi wanaojiriwa kwa mara ya kwanza huchelewa kuthibitishwa na mamlaka; kwa kuunganisha mishahara na akaunti za benki jambo ambalo hupelekea malalamiko ya kukosa mshahara.</p> <p>viii) Mfumo wa Lawson wakati mwingine unafanya kazi taratibu au wakati mwingine haufunguki kabisa.</p>							
2017/18 2.10.2	<p><b>Mapungufu ya mfumo wa Kiuhasibu na utoaji taarifa katika vituo vya kutolea huduma.</b></p> <p>Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri kupitia TAMISEMI ilianzisha mfumo wa Kiuhasibu na Utoaji taarifa katika ngazi ya Vituo vya kutolea huduma (FFARS). Katika kupitia mfumo huu mapungufu kadhaa yameweza kubainika ikiwa ni pamoa na;</p> <p>i) Uelewa mdogo wa watumiaji wa mfumo huu.</p>	<p><b>Ushauri Na. 15</b></p> <p>Tunaitaka Menejimenti kuwasiliana na TAMISEMI ili kutatua changamoto zilizonekana hapo juu ili kupata matokeo chanya ya uanzishwaji wa mfumo huu.</p>	<p>Menejimenti inakubaliana na mapendekezo ya ukaguzi ili kupata juhudii zaidi za kushirikiana na TAMISEMI, changamoto za mifumo zimekuwa zikielekezwa kwa TAMISEMI kupitia msaada wa mtumiaji "Helpdesk" ili zifanyiwe kazi, hata hiyo mapungufu mengi yallyoonekana wakati wa ukaguzi yamefanyiwa kazi na mfumo sasa una tija kama ulivyo kusudiwa. Mafunzo kwa watumiaji mfumo ngazi za vituo vya kutolea hudma (Mashuleni na</p>	<p><b>Zenobi Choka-DICTO TAMISEMI</b></p> <p>Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kutokana na hoja za mapungufu ya mfumo huu.</p>	<p><b>Hoja haijafungwa</b></p>	<p>Halmashauri iendelee kuwasiliana na mamlaka husika ili mapungufu yaliyobainishwa katika mfumo yafanyiwe kazi</p>	<p>Menejimenti iwasiliane na mamlaka husika ili kutatua changamoto zilizobainishwa</p>	<p>Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe</p>

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>ii)Ushirikishwaji mdogo wa watumiaji wa mfumo katika maandalizi ya bajeti hali inayopelekea changamoto nyingi katika matumizi ya bajeti hiyo.</p> <p>iii)Mfumo unafanya kazi ya kudhibiti matumizi ya fedha taslimu lakini hauonyeshi matumizi ya fedha kupitia kwa wazabuni.</p> <p>iv)Mfumo hauna udhibiti wa kutosha ambao unaweza kupelekea kushindwa kudhibiti matumizi ya bajeti kwa kuwa mfumo unatoa ruhusa kwa mtumiaji kufanya mabadiliko katika bajeti wakati ikiendelea kutumika.</p> <p>v)Mfumo kushindwa kutoa taarifa katika fomu tofauti kama vile "Word", "Excel" isipokuwa "PDF" tu.</p> <p>vi)Kutoweza kufanya malipo kwa njia ya masurufu.</p> <p>vii)Mfumo hauwezi kengeneza fomu ya maombi ya manunuzi kutoka ndani ya mfumo badala yake inatumika kutoka nje.</p> <p>viii)Taarifa ya mkeka wa</p>			Vituo nya kutolea huduma za Afya) yametolewa kwao na wanaendelea na matumizi ya mfumo huu. Pia katika maboresho ya mfumo huu, umeunganishwa pamoja na mfumo wa maandalizi ya bajeti "PlanRep" ili kuhakikisha kuwa matumizi ya bajeti za vituo hivi yanaakisi mpango uliopo kwenye mfumo wa maandalizi ya bajeti.				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>matumizi "Cash book" hauonyeshi vifungu vyat matumizi.</p> <p>ix)Mfumo kuwa kufanya kazi taratibu, pia wakati mwingine kuzimika bila utaratibu hali inayowenza kupelekea kupoteza taarifa ambazo zimefanyiwa kazi na hazikuwa zimehifadhiwa.</p> <p>x)Mfumo kushindwa kutoa taarifa halisia kuwa taarifa zinazotolewa hazitoki kwa wakati mpaka ziwe zimetengenezwa mfano ni; Taarifa za mapato na matumizi, taarifa za wafadhili na taarifa za salio.</p>							
2017/1 8 2.10.3	<p><b>Mapungufu katika mfumo wa malipo wa Epicor (IFMS-EPICOR)</b></p> <p>Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inatumia mfumo wa malipo wa malipo wa Epicor 10.2. Sheria namba 11 (2) (d) ya fedha inamtaka Mkurugenzi Mtendaji na Mweka Hazina kuuvezesha mfumo huu wa malipo kufanya kazi ipasavyo. Wakati wa ukaguzi mfumo huu</p>	<p><b>Ushauri Na.16</b></p> <p>Tunashauri Halmashauri kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kushirikiana ili kutatua changamoto hizo.</p>	<p>Uongozi unakubaliana na maoni ya Mkaguzi, hata hivyo uongozi umekwisha wasiliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kutatua changamoto hizo.</p>	<p><b>Lucas Ndombele-Mweka Hazina</b></p> <p>Hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa, hoja imetokana na mapungufu ya mfumo</p>	<p><b>Hoja haijafungwa</b></p>	<p>Halmashauri iendelee kuwasiliana na mamlaka husika ili mapungufu yaliyobainishwa katika mfumo yafanyiwe kazi</p>	<p>Menejimenti iwasiliane na mamlaka husika ili kutatua changamoto zilizobainishwa</p>	<p>Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe</p>

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>umeonekana kuwa na mapungufu yafuatayo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mfumo kushindwa kutoa taarifa sahihi ambazo zinaweza kutumika wakati wa kufunga hesabu za mwisho.</li> <li>• Mfumo wa Epicor 10.2 unafanya kazi taratibu.</li> <li>• Mfumo wa Epicor 10.2 una “asset management module” ambao haujawezeshwa ili utumike.</li> <li>• Mfumo unaenda kinyume na matakwa ya IPSAS</li> </ul>							
2017/18 2.12.1	<b>Usimamizi wa Mapato</b> <b>Kutokusanywa kwa Mapato yatokanayo na Viwanja kutokana na usimamizi usioridhisha wa ukusanyaji Mapato TZS 373,215,430</b> Wakati wa ukaguzi ilibainika Halmashauri ilipima viwanja 72,551 katika eneo la Kitalu "T" liliopo Tukuyu Mjini ambalo lina usajili wa Namba 97317 kwa gharama ya Ths 7,000 kwa mita moja ya mraba kwa ajili ya makazi na matumizi mengine	<b>Ushauri Na.17</b> Tunashauri kuungeza jithada katika ukusanyaji wa mapato ya viwanja	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi, Halmashauri likua na jumla ya viwanja 73 ambapo hapo awali ilifanikiwa kuuza viwanja 21 na kukusanya kiasi cha Ths. 150,517,601.60 Ili kuhakikisha viwanja vyote vinauzika Halmashauri ilitangaza upya uuzaaji wa viwanja 52 ambavyo vilikuwa havijalipiwa ili kupata waombaji wapya. Ambapo viwanja vyote 52 vimepata waombaji na kiasi cha Ths 164,000,000 kinategemewa kukusanya kutokana na mauzo	<b>Mwajuma Kihyo-Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili</b> Halmashauri kupitia kikao cha wataalamu cha 5/3/2020 kimemwelekeza Afisa Ardhi kuhakikisha anafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa viwanja vyote vilivyouzwa.	<b>Hoja haijafungwa</b>	Halmashauri iendelee kuweka msisitizo wa ukusanyaji wa mapato ya mauzo ya viwanja	Menejimenti ihakikishe fedha zote za mapato ya viwanja zinakusanya	Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>ya kijamii.</p> <p>Ambapo Halmashauri ilitegemea kukusanya kiasi cha Tshs.439,644,220 kutokana na mauzo ya viwanja hivyo katika mwaka wa fedha 2017/2018.</p> <p>Hata hivyo kutokana na gharama kubwa za mita moja ya mraba iliyowekwa na Halmashauri, waombaji wa viwanja hivyo walishindwa kuwilipia, na hadi kufikia tarehe 30/6/2018 kiasi cha Tsh.66,428,790 pekee kilikua kimekusanya ambacho ni sawa na 15%</p>		<p>ya viwanja hivyo. Hadi sasa kiasi cha Tshs 91,000,000 kimeshakusanya Rejea viambata husika.</p>					
2017/18 2.16.1.3	<p><b>Kutorejeshwa kwa mikopo katika mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana kutoka katika vikundi kiasi cha Tshs.92,422,500</b></p> <p>Halmashauri imetoa mikopo kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kupunguza umaskini.</p> <p>Hata hivyo katika ukaguzi wa rejista za vikundi vya</p>	<p><b>Ushauri Na. 18</b></p> <p>Tunashauri Menejimenti kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inarejeshwa kwa wakati ili kuruhusu vikundi vingine vya wanawake na vijana kunufaika na mikopo hiyo.</p>	<p>Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi,, Halmashauri imetoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kupunguza umaskini katika utoaji wa mikopo vikundi hufanya marejesho ndani ya miezi 12 kama mikataba inavyoeleza.</p> <p>a) Kwa marejesho ya mikopo uliotolewa mwaka</p>	<p><b>Omari Mungi-DCDO</b></p> <p>Idara ya maendeleo ya jamii imeelekezwa kuitia kikao cha timu ya menejimenti cha tarehe 5/3/2020 kuhakikisha mikopo yote inayotolewa inarejeshwa kwa muda mwafaka</p>	<p><b>Hoja imefungwa</b></p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	mbalimbali zenyenye thamani ya TZS 21,884,784 alifanyika kwa njia ya masurufu maalum. Aidha, baada ya kupitia Mpango wa Manunuzi tulibaini kwamba manunuzi haya yalipangwa kufanyika kwa njia za ushindani na sio kwa njia ya Masurufu kinyume na kifungu Na. 69(8) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016).		pekee. Shajala zilinunuliwa wakati wa zoezi la ufungaji wa hesabu za serikali. Hivyo basi, manunuzi haya yalifanyika kwa njia ya masurufu kwa kuwa yalikuwa manunuzi madogo madogo (micro procurement) kwa mujibu wa kifungu Na. 166(1)&(4) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (kama zilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016). Aidha, manunuzi mengine yalifanyika kwa dharura kutokana na ujio wa Mh. Rais katika Halmashauri yetu ujio ambao haukutarajiwa na Halmashauri na kujua mahitaji kiasi gani yatapaswa kutumika.					
2.15.2	<b>Mapungufu kwenye ujenzi wa vyoo vya umma vilivyogharimu kiasi cha Tsh 28,671,615</b> Wakati wa ukaguzi wa mwaka, Halmashauri iliingia Mkataba na ndugu Reuben Moses Matumba kwa Mkataba Na LGA/071/2018/2019/W/PPP/01 kwa ajili ya kujenga choo cha jumuiya kwenye standi mpya ya Tukuyu mjini kwa ukaribu zaidi ili	<b>Ushauri Na. 52</b> Tunaishuri manejimenti yafuatayo. (a) Kuhakikisha kuwa mikataba yote itakayoingiwa na Halmashauri kwa hapo baadaye inasimamiwa na kufutiliwa kwa ukaribu zaidi ili	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi. Ni kweli Halmashauri ya Rungwe iliingia mkataba na mkandarasi Ndg.Reuben Moses Matumba kwa njia ya ubia (PPP) ili kujenga choo kwa matumizi ya umma kwenye stendi mpya ya Tukuyu mjini kwa mkataba Na.LGA/071/2018/2019/W/PPP/01 kwa gharama ya Tsh 28,671,615.	<b>Mhandisi-Anosisyé Mwasege</b>  Mhandisi wa Wilaya alielekezwa kupitia kikao cha CMT kilichofanyika tarehe 5-3-2020 kuhakikisha anasimamia	<b>Hoja imefungwa</b>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>Sh. 28,671,615. Katika Mkataba huu ,Mkandarasi alitakiwa kuwekeza ujenzi na akusanye mapato ndani ya miaka 10 kama inavyojeleza kwenye kanuni Na 8.1 ya Mktaba.</p> <p>Hata hivyo wakati wa ukaguzi mapungufu yafuatayo yaliweza kuonekana kutokana na zabuni na utekelezaji wa mktaba .</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwenye faili la mkataba ilionekana mkandarasi hakuweza kuwasilisha mpango pendekezwa wa kazi kwa Hal mashauri kulingana na kanuni Na 5.2 (b) (iv) ya mkataba.</li> <li>• Hakukuwa na ufuatiliaji wala usimamizi wa kila mwezi na taarifa za ukaguzi wa ndani wa mradi kulingana na kanuni No.5 (b) (ix) ya makataba.</li> <li>• Hakukuwa na uthibitisho wa kwamba mkandarasi amekamilisha na kupewa hati ya kukamilisha</li> </ul>	<p>kujua thamani halisi ya mradi kwa miradi inayotekeliza.</p> <p>(b) Kuanda taarifa ya uthibitisho na ukaguzi ilikujua gharama ya halisi ya mradi kuwa umegharimu kiasi cha Sh 28,671,615 na muda wa mradi kutumika ndani ya miaka kumi ijayo.</p>	<p>Mapungufu mbalimbali yalijitokeza kutokana Mkandarasi tuliyeingia naye ubia kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusiana na kanuni za mikataba</p> <p>Hata hivyo ukaguzi na ufuatiliaji ulikuwa unafanyika mara kwa mara kwa kushirikiana na mkandarasi na makosa yaliyoweza kuonekana yalitolewa ushauri na kufanyiwa marekebisho</p> <p>Zaidi ya hayo tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi kuzifanyia na tutahakikisha mikataba mingine inasimamiwa ipasavyo. Kwa sasa choo hiko kinatumika baada ya marekebisho kufanyika.</p> <p>.</p>	<p>ipasavyo ujenzi wa choo husika pamoja na kuhakikisha usimamizi madhubuti wa mikataba yote ya ujenzi</p>				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>mradi kabla hajaruhusiwa kuanza kutoa huduma au kufanya biashara kwa muda wa mika 10 kama inavyojeleza kwenya kanuni Na 8.1 ya mkataba.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Hakukuwa na hati ya kukamilisha mradi ambayo imeandaliwa na msimamizi wa mradi kwa mkandarasi ili kuthibitisha kuwa mradi umekamilika kulingana na kanuni Na 4.1 ya makataba..</li> <li>• Katika kufanya tathimini yetu kwa undani hatukuona kwamba makadirio ya mradi (BOQ) ya Sh. 28,671,515 kwa ufanisi yalipitiwa, kusimamiwa na kufanyiwa tathimini ya ubora na thamani ya mradi ( Value for money )</li> </ul> <p>Zaidi ya hayo wakati wa kutembelea mradi tarehe 02/12/2019 katika standi mpya Tukuyu mjini yafuatayo yalioneckana.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mradi ulikuwa bado kukamilika ikiwa na pamoja na kujenga tanki la maji (raiser tank),</li> </ul>							

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>skimming na kupaka rangi kwa jengo lote.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>•Mkandarasi alikuwa anaendelea kutoa huduma bila ya kupewa hati ya kukamilisha ujenzi ambayo inathibitishwa na kutolewa na msimamizi wa mradi.kulingana na kanuni Na 4.1 ya mkataba.</li> <li>• Makusanyo ya ada ya malipo ya choo ya mwezi mmoja uliopita yaliykuwa hayajulikani kwamba yalipokelewa na Halmashauri au mahali pengine bila ya manejimenti kuwa na wasiwasi.</li> </ul>							
2.15.3	<p><b>Ucheleweshwaji wa ukarabati wa mradi wa mradi wa maji Ushirika na Nditu wenyewe thamani ya Tsh. 316,904,400</b></p> <p>Katika mwaka wa ukaguzi, halmashauri iliingia mkataba LGA/071/2017/2018//R/DC/W/1 4 na kampuni ya "M/S Ntoka Company Limited" kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji Ushirika na Nditu kwa gharama ya Tshs. 316,904,400/. Muda wa mkataba wa kufanya kazi ulianza tarehe 12/04/2019 hadi</p>	<p><b>Ushauri Na. 52</b></p> <p>Uongozi wa halmashauri unahimizwa kufuata vifungu vya mikataba na kuongeza kasi ya ufuatilaji na usimamizi, ili kuhakikisha miradi yote ilivoanza inakamilika kama ilivyopangwa kwani kwa sasa wilaya inawatalaamu wa kutosha katika usimamizi wa miradi.</p> <p>Hadi kufikia robo ya tatu ujenzi wa Tanki la kuhifadhi maji umekamilika, ulazaji wa mabomba ya maji safi</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya mkaguzi, Uongozi wa halmashauri utafuata vifungu vya mikataba na kuongeza kasi ya ufuatilaji na usimamizi, ili kuhakikisha miradi yote ilivoanza inakamilika kama ilivyopangwa kwani kwa sasa wilaya inawatalaamu wa kutosha katika usimamizi wa miradi.</p> <p>Hadi kufikia robo ya tatu ujenzi wa Tanki la kuhifadhi maji umekamilika, ulazaji wa mabomba ya maji safi</p>	<p><b>Mhandisi- Vicent Salonga- Meneja RUWASA</b></p>	<p>hoja haijafungwa utekelezaji wa mradi unaendelea</p>	<p>Tunashauri hoja hii ihamishiwe RUWASA ili kurahisisha ufuatilaji.</p>	<p>Mali zote ikiwa ni pamoja na mikataba ya Miradi ya Maji imehamishiwa rasmi RUWASA kuanzia tarehe 01-07-2019 hivyo ni vema hoja hii ikahamishiwa RUWASA</p>	<p>Maoni ya kamati ya fedha yazingatiwe</p>

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>tarehe 13/10/2019 lakini muda wa nyongeza uliongezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza hadi kufikia 30/11/2019 na ya pili hadi 20/01/2020</p> <p>Hata hivyo mapitio ya mpango kazi yaliowasilishwa (Mwezi Oktoba hadi Disemba, 2019) ulionesha kwamba mkandarasi alishatulia miezi miwili nje ya miezi mitatu iliyoongezwa (Muda wa nyongeza), lakini sehemu kubwa ya kazi ilikuwa bado haija kamiliika, kama ilivyonekana wakati wa kutembelea mradi tarehe 2/12/2019.</p> <p>Zaidi, tulibaini mapungufu yafuatayo;</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Wakati wa kutembelea mradi hakuna mfanyakazi ye yeyote aliye kuwepo eneo la kazi na Gari la kubeba maji safi ndio mtambo pekee uliokuwepo eneo la mradi kati ya mitambo yote iliyo orodheshwa,</li> </ul>		<p>unaendelea kufanyika na hadi sasa yamelazwa kilometra 6 kati ya jumla ya kilometra 20.56</p> <p>Halmashauri imeendelea kufatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maji kama ulivyooneleshwa katika majibu husika yaliowasilishwa kupitia barua yenye Kumb Na. CA.3/71/02/08 ya tarehe 02-05-2020</p> <p>Pamoja na majibu ya utekelezaji wa miradi husika, usimamizi wa miradi yote ya Maji kwa sasa umehamishiwa RUWASA kuanzia tarehe 1-07-2019 hii ikiwa ni pamoja na Mikataba na Mali nyinginezo za RUWASA..</p>					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>kinyume na nyaraka za zabuni.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• kinyume na kipengele 3.14 na 3.15 cha mpango kazi uliowasilishwa, mkandarasi hakumalizia shughuli ndogondogo zilizosalia katika vipengele tanjwa</li> <li>• Kinyume na kipengele 2.1, Uungaji wa viungio ulikuwa bado haujafanyika.</li> <li>• Pia tuliona kwa upande wa Ushirika hakuna kazi ilifanyika katika kipengele cha 3.16 cha bomba za chuma na zingine na kipengele cha 3.17 kinachohusu chemba za “valve”</li> </ul>							
2.15.4	<p>Dawa na Vifaa Tiba bila vimepokelewa kukaguliwa vyenye thamani ya TZS 24,846,300</p> <p>Wakati wa ukaguzi wa mwaka</p>	<p>Ushauri Na. 54</p> <p>Menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuongeza udhibiti</p>	<p>Taasisi imekubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba kwa bahati mbaya kipindi cha ukaguzi taarifa ya ukaguzi haikuambatanisha na hati ya malipo hata hivyo Hati ya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba</p>	<p>Dr John Mrina-DMO</p> <p>Mganga Mkuu, ameelekezwa na kikao cha</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	2018/2019, ilibainika kwamba dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya TZS 24,846,300 ambazo zilinunuliwa na kuanza kutumika bila kufanyiwa ukaguzi na timu maalumu ya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba kinyume na kifungu Na. 244 na 245 ya kanuni za manunuvi ya umma ya mwaka 2013 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016). Aidha pia ni kinyume na kifungu Na. 58 (1) & (2) Mwongozo wa Usimamizi wa Fedha, 2009.	wa upokeaji wa vifaa kwa kuhakikisha Timu ya Ukaguzi inaundwa kwa ajili ya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba na kuandaa taarifa ya ukaguzi wa vifaa vyote vilivyonunuliwa iwapo vimekidhi ubora wa viwango kusudiwa.	imeambatanishwa na ipo kwa ajili ya uhakiki.	menejimenti kilichofanyika tarehe 5 Machi, 2020 kuhakikisha anazingatia taratibu za manunuvi katika uagizaji na upokeaji wa dawa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za manunuvi ili kuhakikisha vifaa vyote vinakaguliwa kabla ya kuanza kutumika.				
2.15.5	<b>Vifaa vilivyonunuliwa kwa Mzabuni asiyethibitishwa kiasi cha TZS 90,345,919</b>  Kifungu Na. 131 (4) (b) cha kanuni za manunuvi za mwaka 2013 zinaitaka Taasisi Nunuzi kununua bidhaa mtambua kutoka kwa wazabuni walioihinishwa na kuingia mkataba na Wakala wa Huduma ya Ununuvi Serikalini kwa kuwapelekea oda za manunuvi baada ya	Ushauri Na. 55 Menejimenti ya Halmashauri inakubaliana na maoni ya mkaguzi hata hivyo, mzabuni Wintu Company Limited alipitishwa na Wakala wa Ununuvi Serikalini (GPSA). Nakala ya mkataba ipo kwa ajili ya uhakiki.	Menejimenti ya Halmashauri inakubaliana na maoni ya mkaguzi hata hivyo, mzabuni Wintu Company Limited alipitishwa na Wakala wa Ununuvi Serikalini (GPSA). Nakala ya mkataba ipo kwa ajili ya uhakiki.	<b>Victor Mwakapala-HPMU Dr.John Mrina-DMO</b>  Mganga Mkuu na Afisa Manunuvi wameelekezwa na Menejimenti kupitia kikao cha tarehe 05/03/2020 kuhakikisha muda wote wa kufanya manunuvi	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>kuidhinishwa na Afisa Masuhuli/ au mtumishi mwingine aliyezasimiwa madaraka. Aidha, kanuni ya namba 55(7) ya PPR 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2016 iliitaka menejimenti kuwasilisha orodha ya wazabuni waliopitishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini na kuthibitishwa na Bodi ya Zabuni.</p> <p>Hata hivyo, wakati wa ukaguzi katika Hospitari ya Wilaya na kituo cha Afya Masukulu tulibaini manunuzi yenyenye Jumla ya Tsh 90,345,919 ambayo yalifanyika kwa wazabuni ambao hawajasajiliwa na wakala wa manunuzi Serikalini na hawapo kwenye orodha.</p>	thamani ya fedha inapatikana.		wanazingatia sheria, taratibu na kanuni za Manunuzi kwa kuhakikisha wanatumia wazabuni walipitishwa na Mamlaka husika.				
2.15.6	<p><b>Kutotumika ipasavyo kwa Oda ya Manunuzi wakati wa kuagiza mafuta yenyenye thamani ya TZS 17,646,885</b></p> <p>Kanuni Na. 164(2)(j) ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama ilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016</p>	<p>Ushauri Na. 56</p> <p>Menejimenti inashauriwa kuongeza udhibiti wa manunuzi ya mafuta kwa</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya mkaguzi; mapungufu hayo yalitokana na muaandaji wa Oda ya Manunuzi kushindwa kugawanya vizuri kiasi cha fedha iliyotengwa ukilinganisha na bei ya mafuta ilijoazwa na mzabuni kwenye mfumo wa epicor</p>	<p><b>Victor Mwakapala-HPMU</b></p> <p>Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi ameelekezwa kuzingatia taratibu za manunuzi wakati</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>inaitaka Taasisi Nunuzi kuandaa makubaliano ya mkataba au Oda ya Manunuzi (LPO) kwa kujumuisha masharti yote ya mkataba, maelezo ya sarafu itakayotumika wakati wa kumlipa mzabuni au mkandarasi iwapo itakuwa tofauti na alijojaza mzabuni kama iliyoelezwa na kifungu cha Mwongozo wa Usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa Na. 69(1) za mwaka 2009.</p> <p>Hata hivyo, wakati wa ukaguzi tulibaini kuwa Halmashauri ilianda Oda za Manunuzi (LPO) za Mafuta zenye thamani ya TZS 17,646,885 ambazo zinakosa maelezo muhimu ya idadi halisi ya lita zilizoagizwa na bei kwa kila lita ya mafuta kwa mujibu wa hati ya madai zilizoambatanishwa.</p>	<p>kuhakikisha kwamba manunuzi yote lazima yaoneshe uhalisia wa kiasi kinachoagizwa bei kwa kila kimoja.</p>	<p>kutokana na baadhi ya vifungu vilitengewa fedha kidogo kidogo kiasi cha kushindwa kugawanya kwa kila bei ya lita moja ya mafuta. Lakini pia baadhi ya Wafadhilli hawaruhusu kubakiwa na fedha katika akaunti katika vifungu husika mfano fedha za UNICEF, Walter Reed n.k. Hata hivyo, kwa sasa udhibiti umeimarishwa ambapo oda za manunuzi zimezingatia ushauri wa mkaguzi na kwamba nakala za Oda za Manunuzi zipo kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p>wa kuandaa Oda za Manunuzi kupitia kikao cha 05/03/2020.</p>				
2.15.7	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kusainiwa kwa Hati ya mapokezi (receipt vouchers) na Wakuu wa Idara zenye thamani ya TZS 10,362,998	<p>Ushauri Na. 57 Menejimenti inashauriwa kuhakikisha inaongeza udhibiti katika upokeaji wa</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya Mkaguzi, hata hivyo hati za mapeokezi zilizohojiwa zimeshasainiwa na Wakuu wa Idara/Vitengo husika na kwamba zipo kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p>Victor Mwakapala-HPMU Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi ameelekezwa</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>Aya No.16.2 ya Mwongozo wa Usimamizi wa fedha wa mwaka, 2009 unataka vifaa viliv yokaguliwa na kupokelewa na Timu ya Ukaguzi kupokelewa na Afisa Ugavi ambaye ataingiza kumbukumbu za mapokezi ya vifaa hivyo kwenye kitabu cha Hati ya kupokelea vifaa (GRN/Stores Receipt Voucher).</p> <p>Pamoja na kujaza kumbukumbu hizo Hati ya mapokezi ya vifaa inapaswa kusainiwa na Afisa Ugavi na Mkuu wa Idara aliyegiza vifaa Hata hivyo, wakati wa ukaguzi tulibaini vifaa vyenye thamani ya TZS 10,362,998 vilinunuliwa na kupokelewa ingawa havikusainiwa na Wakuu wa Idara/Vitengo kwa ajili ya kuthibitisha upokeaji wa vifaa hivyo kinyume na aya iliyotajwa hapo juu.</p>	vifaa vinavyonunuliwa kwa kuwasainisha Wakuu wa Idara/Vitengo ili kujiridhisha na manunuzi yaliyofanyika.		kuzingatia taratibu za manunuzi wakati wa mapokezi ya vifaa kupitia kikao cha 05/03/2020.				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
-------------	-----------------	---------------------------	-------------------	--	------------------------	----------------------------------	--------------------------------	--------------------------------------

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### HOJA ZA MFUKO WA PAMOJA WA AFYA

2.1	Hali ya kifedha	Ushauri Na.1	Uongozi wa halmashauri unakubaliana na ushauri wa mkaguzi. Hoja hii imetokana na fedha za Mfuko wa Afya kufika kwa kuchelewa. Halmashauri itaendelea kuwasiliana na Mamlaka husika ili kuhakikisha fedha husika zinaletwa kwa wakati kulingana na bajeti iliyopangwa. Kwa sasa fedha hizo zimeshatumika kwa shughuli zilizopangwa.	Dr John Mrina-DMO	Hoja imefungwa			
2.1.1	Kiasi cha fedha ambazo hazikutumika chenye thamani ya Tshs. 107,612,798  Wakati wa ukaguzi halmashauri ilikuwa na jumla ya kiasi cha fedha Tshs.540,852,708 za mfuko wa pamoja wa afya zilizokuwa zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za idara ya afya, ikiwa ni pamoja na salio anzia Tshs. 21,947,108 hata hivyo kufikia tarehe 30 Juni, 2019 halmashauri ilitumia kiasi cha Tshs.433,239,910 sawa na asilimia 80 na kuwa na bakaa ya Tshs.107,612,798	Uongozi wa halmashauri ulishauriwa kuhakikisha fedha ambazo zilibaki zinatumika ili kukamilisha shughuli kama zilivyopangwa zaidi Mweka hazina anashauriwa kutoa fedha mapema kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa wakati.	Mganga Mkuu alielekezwa kwenye kikao cha timu ya uongozi wa Halmashauri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2020 kutumia fedha zote zilizobaki kama iliyopangwa kwenye bajeti					

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
2.2 2.2.1	<p><b>Hali ya uendeshaji</b></p> <p><b>Kutowasilishwa kwa mpango na bajeti ya idara ya afya pamoja taarifa za robo mwaka za fedha na utekelezaji katika Sekretariati ya Mkoa.</b></p> <p>Kifungo kidogo Na 4.4.6 cha mwongozo wa mpango na bajeti wa mwaka 2011 unasema mweka hazina wa halmashauri atatoa taarifa kila mwezi kwenye kamati ya fedha utekelezaji wa huduma za afya. Akionyesha mapato, matumizi na bakaa kwa fedha zote zilizotolewa kwa halmashauri. Taarifa itaambatanishwa na taarifa ya benki, usuluhishi wa kibenki na cheti kinachoonyesha bakaa. Halmashauri tena itawasilisha taarifa ya robo Sekretariat ya mkoa kwa ukaguzi na kuiwasilisha Ofisi ya Rais tawala za mikoa na serikali za pia pamoja na wiazara ya afya. Hata hivyo timu ya ukaguzi ilipitia nyaraka kutoka uongozi wa halmashauri iligundua</p>	<p><b>Ushauri Na.2</b></p> <p>Uongozi wa halmashauri ulishauriwa</p> <p>(a) Kuimaris ha usimamizi wa ndani juu ya uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji.</p> <p>(b) Kutoa vidhibitisho vya kutosha kushindwa kufuata utaratibu wa kuwasilisha taarifa.</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya mkaguzi Ofisi ya Rais-Tamisemi iliunganisha mifumo ya PLANREP, FFRAS na EPICOR hivyo taarifa mbalimbali za fedha zinapatikana kiurahisi kwa kuingia kwenye mfumo wa PLANREP. Hata hivyo Menejimenti imetoa nakala ngumu na kuiwasilisha katika Ofisi za Sekretariat ya Mkoa na zipo tayari kwa uhakiki.</p>	<p><b>Dr John Mrina-DMO</b></p> <p>Mganga mkuu alielekezwa kwenye kikao cha timu ya uongozi wa halmashauri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2020 kuhakikisha taarifa hizo zinawasilishwa kwa wakati.</p>	<p><b>Hoja imefungwa</b></p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	hakuna nyaraka zozote za udhibitisho kuonyesha taarifa za fedha za robo zilizoandaliwa hazikuwasilishwa Sekretariat ya mkoa kwa ukaguzi kwani hakukuwa na nyaraka yoyote ya udhibitisho.							
2.3	Manunuzi na Usimamizi wa mikataba  Vifaa vilivyonunuliwa vilipokelewa bila kukaguliwa vyenye thamani ya TZS 3,381,240  Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/2019, ilibainika kwamba dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya TZS 3,381,240 vilinunuliwa na kuanza kutumika bila kukaguliwa na Kamati ya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba (therapeutic team), kinyume na kifungu Na. 58 (1) & (2) Mwongozo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali za Mitaa za mwaka, 2009 na kanuni Na. 245 Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2013 (kama ilivyofanyiwa marekebisho, 2016).	Ushauri Na. 3  Halmashauri inashauriwa kuongeza udhibiti tika upokeaji wa vifaa ili kuhakikisha ukaguzi a mali zinazonunuliwa unafanyika kabla ya kuanza matumizi ya mali hizo.	Halmashauri inakubaliana na maoni ya mkaguzi hata hivyo taarifa ya ukaguzi ya manunzi ya dawa na vifaa tiba ambayo kwa bahati haikoambatanisha na nyaraka za malipo ipo kwa ajili ya uhakiki.	Dr John Mrina- DMO  Mganga Mkuu ameelekezwa kupitia kikao cha tarehe 05 Machi, 2020 kuhakikisha anazingatia sheria na kanuni za manunuzi katika ununuvi wa dawa na vifaa tiba kwa kuhakikisha dawa na vifaa tiba zilizounuliwa zinakaguliwa kabla ya kuanza kutumika.	Hoja imefungwa			
2.3.1								

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
2.3.2	<p>Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya manunuzi vifaa na huduma pasipo kuandaliwa Oda za Manunuzi au mikataba mdogo ya manunuzi yenye thamani ya TZS 50,499,643</p> <p>Kanuni Na. 160(g) na 164 (1)(2)(j) za manunuzi ya umma ya mwaka 2013 (kama iliyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016) zinaitaka Taasisi Nunuzi kuandaa Oda ya Manunuzi au mikataba mdogo utakaohusisha masharti yote ya mikataba, maelezo ya sarafu itakayotumika wakati wa kumlipa mzabuni au mkandarasi iwapo itakuwa tofauti na alijojaza mzabuni.</p> <p>Hata hivyo, wakati wa kupitia hati mbalimbali za malipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe tulibaini kwamba jumla ya kiasi cha TZS 50,499,643 kililipwa kwa wazabuni mbalimbali bila kuandaliwa kwa Oda za Manunuzi ambazo</p>	<p>Ushauri Na. 4</p> <p>Menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuhakikisha manunuzi yote ya vifaa yanaambatana na Oda za Manunuzi au mikataba mdogo ya manunuzi ambayo inaelezea masharti maalum ya mikataba na namna ya kufanya malipo.</p>	<p>Menejimenti inakubaliana na maoni ya mkaguzi, Oda za Manunuzi husika ambazo hazikuonekana wakati wa ukaguzi zipo kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p>Dr John Mrina-DMO</p> <p>Mganga Mkuu ameelekezwa kupitia kikao cha tarehe 05 Machi, 2020 kuhakikisha anazingatia sheria na kanuni za manunuzi katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa kuhakikisha dawa na vifaa tiba zinanunuliwa baada ya kuandaa Oda za Manunuzi au Mikataba mdogo ya Manunuzi.</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	zinaeleza masharti mbalimbali ya mikataba ya manunuzi.							
2.3.3	<p>Kutotumika ipasavyo kwa Oda ya Manunuzi wakati wa kuagiza mafuta yenyeye thamani ya TZS 7,078,400 Kanuni Na. 164(2) (j) ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016) inaitaka Taasisi Nunuzi kuandaa makubaliano ya mkataba au Oda ya Manunuzi (LPO) kwa kujumuisha masharti yote ya mkataba, maelezo ya sarafu itakayotumika wakati wa kumlipa mzabuni au mkandarasi iwapo itakuwa tofauti na aliyojaza mzabuni kama ilivyoelezwa na kifungu cha Mwongozo wa Usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa Na. 69(1) za mwaka 2009.</p> <p>Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund) tulibaini kuwa Idara ya Afya iliandaan Oda za Manunuzi (LPO) za Mafuta zenyeye thamani ya TZS</p>	<p><b>Ushauri Na. 5</b> Menejimenti inashauriwa kuongeza udhibiti wa manunuzi ya mafuta kwa kuhakikisha kwamba manunuzi yote lazima yaoneshe uhalisia wa kiasi kinachoagizwa bei kwa kila kimoja.</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya mkaguzi; mapungufu hayo yalitokana na muaandaji wa Oda ya Manunuzi kushindwa kugawanya vizuri kiasi cha fedha iliyotengwa ukilinganisha na bei ya mafuta ilijoazwa na mzabuni kwenye mfumo wa epicor kutokana na baadhi ya vifungu vilitengewa fedha kidogo kidogo kiasi cha kushindwa kugawanya kwa kila bei ya lita moja ya mafuta. Lakini pia baadhi ya Wafadhili hawaruhusu kubakiwa na fedha katika akaunti katika vifungu husika mfano fedha za UNICEF, Walter Reed n.k. Hata hivyo, kwa sasa udhibiti umeimarishwa ambapo oda za manunuzi zimezingatia ushauri wa mkaguzi na kwamba nakala za Oda za Manunuzi zipo kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p><b>Victor A. Mwakapala-HPMU</b> Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi ameelekezwa kuitia kikao cha tarehe 05 Machi, 2020 kuhakikisha anazingatia sheria na kanuni za manunuzi</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	7,078,400 ambazo zinakosa maelezo muhimu ya idadi halisi ya lita zilizoagizwa na bei kwa kila lita ya mafuta kwa mujibu wa hati ya madai zilizoambatanishwa.							
2.3.4	<p><b>Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni yenye thamani ya TZS 6,408,800</b></p> <p>Katika kuzingatia matakwa ya kifungu Na. 35(3) cha Sheria Na. 7 za mwaka 2011 na Kanuni Na. 55 ya Manunuzi ya Umma, 2013 vinavyohusu uidhinishaji wa zabuni kupitia Bodi ya Zabuni, tulibaini kwamba Halmashauri imefanya manunuzi ya vifaa na huduma zeny kiasi cha Tsh 6,408,800 bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni.</p>	<p><b>Ushauri Na. 6</b></p> <p>Halmashauri inashauriwa kuongeza udhibiti wa manunuzi ya vifaa na huduma. Aidha, Halmashauri inatakiwa kuzingatia ipasavyo taratibu za manunuzi kwa kuhakikisha Bodi ya Zabuni inashirikishwa ipasavyo katika manunuzi ya Halmashauri ili kuepusha mikataba mibovu au isiyoteklezeka.</p>	<p>Tunakubaliana na maoni ya mkaguzi; hata hivyo manunuzi hayo yalikuwa manunuzi madogo madogo (micro value procurement) kwa mujibu wa kifungu Na. 166 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 (kama ilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2016) ambayo hayakufikia ukomo wa kuweza kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.</p>	<p><b>Dr John Mrina-DMO</b></p> <p>Mganga ameelekezwa kupitia kikao cha tarehe 05 Machi, 2020 kuhakikisha anazingatia sheria na kanuni za manunuzi.</p>	<p><b>Hoja imefungwa</b></p>			
2.4 2.4.1	<b>Usimamizi wa Matumizi Malipo yaliyofanyika bila</b>	<b>Ushauri Na. 7</b>	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi, uongozi umeendelea kuhakikisha taratibu za malipo	<b>Dr John Mrina-DMO</b>	<p><b>Hoja imefungwa</b></p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p><b>kufanyika kwa ukaguzi wa awali ya kiasi cha Tshs.22,132,400</b>  Kifungu Na. 2.4.2 cha memoranda ya Fedha ya Sheria ya Serikali za mitaa ya 2009 inataka hati za malipo na nakala halisi za malipo kupitia idara ya fedha kwa ajili kufanyiwa ukaguzi wa awali ili kujiridhisha na usahihi wa nyaraka husika.</p> <p>Wakati wa ukaguzi ilibaini Malipo ya kiasi cha Tshs 22,132,400 yaliyofanyika kwenye mfuko wa afya wa pamoja yalifanyika pasipo kupita kwenye ukaguzi wa awali.</p>	unashauri kuhakikisha malipo yeto yanafanyiwa ukaguzi wa awali kabla ya kulipwa.	zinazingatiwa ikiwa ni pamoja na kumwandikia barua Mhasibu wa Matumizi yenyne Kumb Na. RDC/F2/29/VOLIII/179 ya tarehe 8-09-2019 kuhakikisha hakuna Malipo yatakayofanyika bila kupitia ukaguzi wa awali ili kuhakikisha usahihi wa Malipo husika na utimilifu wa viambata.	Mganga mkuu alielekezwa kwenye kikao cha timu ya uongozi wa halmashauri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2020 kuhakikisha malipo yote yananyiwa ukaguzi wa awali.				
2.4.2	<p><b>Malipo yenyne nyaraka pungufu ya kiasi cha Tshs. 26,965,994</b>  Kifungu Na. 95(4) cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2001 inasema, hati za malipo ambazo hazijakamilika kwa kukosa viambata, itaainishwa kama hati ambazo hazipo</p>	<b>Ushauri Na.8</b> Uongozi wa hospitali kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha mfumo wa usimamizi kumbukumbu na kutafuta nyaraka zote ambazo hazikuonekana na kuziwasilisha kwa	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi, uongozi wa hospitali ulifanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa kwa kuhakikisha viambata vyote viliviyokosekanavinaambatanishwa kwenye hati za Malipo husika. Hati hizo za Malipo zipo tayari kwa ajili ya uhakiki.	<b>Dr John Mrina-DMO</b> Mganga mkuu alielekezwa kwenye kikao cha timu ya uongozi wa halmashauri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2020 kuhakikisha	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	Wakati wa ukaguzi tuligundua halmashauri kupitia mfuko wa afya wa pamoja ilifanya malipo ya kiasi cha Tshs.26,965,994 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali bila ya kuwa na viambata vya kutosha mfano stakabadhi za kukiri mapokezi, barua za mwaliko na rejestra ya mahudhurio.	ajili ya uhakiki.		anaboresha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za malipo katika hospitali ya Wilaya.				
2.4.3	<b>Malipo ya posho yaliyofanyika bila fomu za madai kwa wahusika yenye thamani ya Tshs. 12,995,000</b> Kifungu Na. 2.4.4 cha memorandamu ya sheria ya serikali za mitaa ya mwaka, 2010 inataka mamlaka za mitaa kuhakikisha kabla ya kufanya malipo yoyote mlipwaji anatakiwa adai kwenye mamlaka akiainisha sababu za malipo yake. Hata hivyo, Wakati wa ukaguzi tuligundua halmashauri ilifanya malipo yenye thamani ya Tshs. 12,995,000 kwa watumishi mbalimbali bila kujaza fomu binafsi za madai kinyume na sheria iliyoainishwa hapo juu.	<b>Ushauri Na. 9</b> Tunashauri Uongozi wa hospitali kuhakikisha kabla kufanyika kwa malipo yanayohusiana na posho yaambatanishwe na fomu za maombi za madai binafsi kama ilivyoainishwa kwenye kifungu Na.2.4. cha memoranda ya sheria ya serikali za mitaa ya mwaka, 2010	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi. Uongozi wa hospitali utaendelea kuhakikisha uzingatiwaji wa taratibu za fedha katika Malipo mbalimbali yanayofanyika. Fomu za madai ambazo hazikuambatanishwa kwenye hati za Malipo zimeshaambatanishwa na zipo tayari kwa uhakiki.	<b>Dr John Mrina- DMO</b> Mganga mkuu alielekezwa kwenye kikao cha timu ya uongozi wa halmashauri kilichofanyika tarehe 5 Machi 2020 kuhakikisha madai yote yanahusiana na posho yanakuwa na fomu za madai binafsi.	<b>Hoja imefungwa</b>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
-------------	-----------------	---------------------------	-------------------	--	------------------------	----------------------------------	--------------------------------	--------------------------------------

### HOJA ZA SEKTA YA MAJI

2.1	Muhtasari wa Kifedha	Ushauri Na.1	Tunakubaliana na ushauri wa Mkaguzi, fedha zilizokuwa hazijatumika kiasi cha zisizotumika kiasi cha Tsh 2,783,489 ziliingizwa katika bajeti ya shughuli za matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2019/2020 na fedha zote zimeshatumika. Rejea kiambata husika	Mhandisi-Vincent Saronga-Meneja RUWASA	Hoja imefungwa			
2.1.1	Fedha za WSDP zisizotumika Tsh 2,783,489  Kwa kipindi cha mwaka wa ukaguzi, halmashauri ilikuwa na jumla ya fedha kiasi cha TZS 3,379,723,165 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Shughuli za Maendeleo ya Sekta ya Maji zikihusisha salio anzia kiasi cha Tsh 63,063,203. Hata hivyo hadi kufikia Juni 30, 2019 Halmashauri imetumia kiasi cha Tsh 3,376,939,677 sawa na 99%	Menejimenti ya HalmaShauri inashauri kuwa manunuza na mikataba yao inasimamiwa ipasavyo ili kuharakisha matumizi ya fedha zisizotumika za WSDP	Barua yenyenye Kumb: Na. RDC/F2/66/40 ya tarehe 23 Machi, 2020 imeandikwa kwa Meneja wa RUWASA kuzingatia na kuwasilisha majibu ya Menejimenti juu ya hoja zitolewazo za WSDP					
2.2	Manunuza na Usimamizi wa mikataba							
2.2.1	Mapungufu yaliyoonekana wakati wa kupitia mafaili ya mikataba mbalimbali  Wakati wa ukaguzi, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe iliingia mikataba mbalimbali na wazabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya							

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	maji kupitia program ya Uendelezaji wa Maji (WSDP).  Hata hivyo, katika mikataba mitatu tulioweza kupitia na nyaraka zinazohusiana na miradi hii tulibaini mapungufu yafuatayo:-							
2.2.1.1	<b>Manunuzi ya mabomba yasiyofuata ipasavyo taratibu za manunuzi yenyenye thamani ya TZS 54,025,037</b>  Mwongozo namba 70 ya usimamizi wa fedha za serikali za mitaa iliitaka Halmashauri kupitia kila mkuu wa idara kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazopokelewa zinakaguliwa sambamba na kuangalia bei, ubora na idadi yake. Pia mwongozo huo 8(2),(c) unamtaka Mweka Hazina kuweka vizuri kumbukumbu zake na viambata vyote vinavyohusiana na malipo. Pia mwongozo namba 77(1) unawataka Maafisa Ugavi wahakikishe wanashughulikia ipasavyo manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa njia ya	<b>Ushauri Na. 2</b> Mnejimenti inashauriwa kuongeza udhibiti wa ndani wa utunzaji wa kumbukumbu sahihi zinazotakiwa, kuongeza utendaji kazi wa Kitengo cha Manunuzi na kuhakikisha nyaraka zote zilizokosekana zinapatikana na kuhakikiwa na mkaguzi.	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi <ul style="list-style-type: none"> <li>Fomu ya maombi ya ununuzi ya awali iliandaliwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018 sambamba na nukuu za hati msako (Proforma invoice) kutoka kiwandani ingawa taratibu za manunuzi zilisimama kutokana na kufungwa kwa mfumo wa Epicor na ndio maana iliandaliwa fomu mpya ya maombi ya ununuzi iliyowekwa vifungu vipyta vya malipo ambayo iliandaliwa mnamo tarehe 12/09/2018 na kuendelea na taratibu zingine za ununuzi wa mabomba hayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.</li> <li>Hati ya mapokezi ya vifaa na</li> </ul>	<b>Mhandisi Vincent Saronga-Meneja RUWASA</b> Barua yenyenye kumb. Na RDC/F2/66/40 ya tarehe 23 Machi,2020 imeandikwa kwenda kwa Meneja wa Maji RUWASA kuhakikisha anazingatia taratibu katika utekelezaji wa manunuzi mbalimbali ya vifaa.	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>tenda.</p> <p>Wakati wa ukaguzi wa hati za malipo katika akaunti ya maji tumegundua kuwa kuna malipo yamefanyika kwa mzabuni PLASCO LIMITED kwa ajili ya ununuzi wa mabomba na vifaa vya vya maji vyenye jumla ya Tsh 54,025,037 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji Kalalo.</p> <p>Hata hivyo wakati wa ukaguzi huo tulibaini kuwepo kwa mapungufu yafuatayo:-</p> <p>i. Fomu ya maombi ya ununuzi iliombwa tarehe 12/09/2018 na kuidhinishwa tarehe 14/09/2018 wakati nukuu ya hati ya awali (Pro-forma invoice) ilikuwa ni ya tarehe 27/06/2018 tarehe ambayo ni kabla ya kuandaa fomu ya maombi kinyume na kifungu Na. 71 (1) ya Mwongozo wa Usimamizi wa fedha za Serikali za mitaa za mwaka, 2009.</p> <p>ii. Kuna uandaaji usiyordhisha wa taarifa ya ukaguzi wa</p>			<ul style="list-style-type: none"> <li>• Hati ya malipo ipo kwa ajili ya uhakiki wa mkaguzi.</li> <li>• Taarifa ya ukaguzi na upokeaji wa vifaa inayoonesha idadi ya vifaa vilivyopokelewa na maeleo ya ubora ipo kwa ajili ya uhakiki.</li> <li>• Stakabadhi ya kielektroniki ya kukiri malipo ya kiwanda cha Plasco Co. Ltd ipo kwa ajili ya uhakiki.</li> </ul>				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>mapokezi ya mabomba hayo kwa kuwa taarifa haikuweza kuonesha idadi ya mabomba yaliyopokelewa ukilinganisha na idadi ya mabomba yaliyoagizwa na iwapo yamekidhi ubora uliotakiwa kwa mujibu wa sifa zinazotakiwa. Kama ilivyoandikwa LPO No.10084 ya tarehe 14/11/2018 kinyume na kifungu Na. 58 Mwongozo wa Usimamizi wa fedha za Serikali za mitaa za mwaka, 2009.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>Aidha, hapakuwa na risiti ya kielektroniki ili kujiridhirisha iwapo kiasi cha fedha kilicholipwa kilimfikia mzabuni husika.</li> </ul>							
2.2.1.2	<p><b>Kutokuwepo na kutoandaliwa kwa taarifa ya ukaguzi ya upokeaji wa vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya TZS 9,773,500</b></p> <p>Vifungu Na. 244 na 245 cha Kanuni za manunuzi ya Umma za 2013 vinataka Afisa Masuuli kuunda na Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya vifaa ili</p>	<p><b>Ushauri Na. 3</b> Menejimenti ya HalmaShauri inashauriwa kuhakikisha Kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa iliyoteuliwa inatekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kuhakikisha</p>	<p>Menejimenti inakubaliana na maoni ya mkaguzi, hata hiyo taarifa ya ukaguzi yenyenayooonesha idadi ya vifaa vilivyopokelewa kwa mujibu wa oda ya manunuzi na hati ya mapokezi kama ilivyo pia kwa sifa kusudiwa zipo kwa ajili ya uhakiki.</p>	<p><b>Mhandisi-Vincent Saronga-Meneja RUWASA</b> Barua yenye kumb. Na RDC/F2/66/40 ya tarehe 23 Machi, 2020 imeandikwa kwenda kwa Meneja wa Maji RUWASA kuhakikisha anazingatia taratibu</p>	<p><b>Hoja imefungwa</b></p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>kujiridhisha na Idadi ya vifaa, ubora na usahihi wa vifaa husika.</p> <p>Wakati wa ukaguzi, tulibaini kwamba Halmashauri imenunua vifaa vya maji vyenye thamani ya TZS 9,773,500. Vifaa hivyo vilipokelewa na kutumika na menejimenti. Hata hivyo, baada ya kupitia kwa kina taarifa ya ukaguzi wa vifaa hivyo, taarifa imeonesha kwamba haikuonesha idadi halisi ya kiasi kilichopokelewa ukilinganisha na Oda ya Manunuzi na Hati ya Mapokezi ili kujiridhisha iwapo kiasi kilichopokelewa kinalingana na oda ya manunuzi.</p>	<p>inaandaa taarifa ya mapokezi ilijoitosheleza kwa mujibu wa sifa za vifaa na ubora unaotakiwa. Aidha, taarifa ya vifaa vyenye thamani ya TZS 9,773,500 inapaswa kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki zaidi.</p>		<p>katika utekelezaji wa manunuzi mbalimbali ya vifaa.</p>				
2.3	<p><b>Utekelezaji wa bajeti</b></p> <p><b>Mapokezi ya fedha za zaidi ya bajeti ya WSDP TZS 891,059,962</b></p> <p>Kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa uhakiki, Halmashauri ilikuwa imepanga kutekeleza</p>	<p><b>Ushauri Na.4</b></p> <p>Menejimenti ya Halmashauri kwa kushirikiana na PO-RALG inasisitizwa kuwasiliana na Hazina pamoja na Wizara ya Maji juu</p>	<p>Menejimenti imekubaliana na ushauri. Kibali cha kutumia fedha zilizopokelewa zaidi ya bajeti jumla ya TZS 682,559,398.54 kimepatikana kupitia kikao cha Kamati ya Fedha cha tarehe 12/04/2019 Muhtasari Na.102/FUM.10/2018/2019</p>	<p><b>Mhandisi-Vincent Saronga-Meneja RUWASA</b></p> <p>Barua yenye Kumb: Na. RDC/F2/66/40 ya tarehe 23 Machi, 2020 imeandikwa kwa Meneja wa RUWASA</p>	<p>Hoja imefungwa</p>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	shughuli mbalimbali zenyet thamani ya TZS 2,425,600,000 kupitia fedha za RWSSP. Hata hivyo hadi kufikia 30 June, 2019 TZS 3,316,659,962 ziliwa zimepokelewa ambapo ilipelekea kupokea zaidi ya TZS 891,059,962 sawa na 37 asilimia ya bajeti husika	ya mapokezi ya fedha za WSDP zaidi ya bajeti; hata hivyo kipatikane kibali na mchanganuo wa kina wa matumizi na kuwasilishwa kwa ajili ya kuthibitishwa.		kuzingatia na kuwasilisha majibu ya Menejimenti juu ya hoja zitolewazo za WSDP				
2.4	<b>Usimamizi wa Matumizi</b>  <b>Malipo yasiyothibitishwa ya posho ya masaa ya ziada kufanyika bila kuonesha muda maalumu kwenye fomu za posho ya masaa ya ziada TZS 14,025,000</b>  Aya 2.4.4 ya LAAM, 2010 inahitaji mamlaka ya serikali za mitaa kuhakikisha kuwa kabla ya mamlaka yoyote ya mtaa kufanya malipo yoyote kwa mlipwaji apeleke maombi kwa mamlaka akionesha sababu ya malipo hayo. Kwa sababu ya isimamizi mzuri wa kifedha fomu za maombi zinasanifiwa kwa misingi maalumu na kukamilishwa na mlipwaji	<b>Ushauri Na.5</b>  Menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuhakikisha kuwa, kabla ya kufanya malipo yahusianayo na posho ya masaa ya ziada inatakiwa kukamilisha ujazaji wa fomu za posho zikionesha muda kama inavyofafanuliwa katika aya 2.4.4 ya LAAM, 2010 na mwongozo Na.78 (1) wa LGFM, 2009 kama	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi Fomu za malipo ya masaa ya ziada zilijazwa bila kuonesha muda kwa kila kazi husika kwa kuwa fomu hizo hazikuonesha sehemu ya kujaza muda kwa kila kazi husika. Hata hivyo, Menejimenti ya Halmashauri itaboresha fomu za malipo ya posho ya masaa ya ziada kwa kuingiza kipengele cha kujaza muda/tarehe kwa kila kazi husika.	<b>Mhandisi-Vincent Saronga-Meneja RUWASA</b>  Barua yenyen Kumb: Na. RDC/F2/66/40 ya tarehe 23 Machi, 2020 imeandikwa kwa Meneja wa RUWASA kuzingatia na kuwasilisha majibu ya Menejimenti juu ya hoja zitolewazo za WSDP	Hoja imefungwa			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIWA KWA WAHUSIKA WALIOSABABISHA A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>baada ya malipo kufanyika. Kwa kipindi cha ukaguzi tulibaini kuwa Halmashauri ilifanya malipo ya masaa ya ziada yenye thamani ya TZS 14,025,000 kwa watumishi mbalimbali wa Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri. Hata hivyo, tulibaini kuwa Halmashauri ilikamilisha fomu za maombi lakini haikuonesha muda wa siku zilizolipwa na baadhi ya malipo yalifanyika bila kukamilisha ujazaji wa fomu za malipo ya masaa ya ziada na kuidhinishwa kinyume na mwongozo 78 (1) wa LGFM, 2</p>	<p>ilivyooneshwa hapo juu. Uhalali wa malipo ya TZS 14,025,000 inapaswa uthibitishwe.</p>						

#### HOJA ZA MFUKO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF)

2.2 2.2.1	<b>UANDAAJI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI</b>  <b>Mapokezi ya fedha kutoka TASAF Makao Makuu pungufu ya bajeti kiasi cha Tshs 1,204,195,450/=</b>	<b>Ushauri Na.1</b> Tunashauri TASAF Makao Makuu (TMU) kuzingatia mkataba uliopo baina ya TMU na Eneo la utekelezaji wa Mpango (PAA) ili kufikia malengo ya kuwakwamua	Managementi inakubaliana na kutopokea hizo fedha Tshs 1,204,195,450/= hii ni kutokana na shughuli iliyojitekeza katikati ya utekelezaji wa Mpango ambayo ilikuwa ni maandalizi ya TASAF awamu ya tatu hatua ya pili ambavyo ilipelekea kusimama kwa utekelezaji wa Mpango ili kupisha zoezi la uhakiki wa	<b>Lydia Mwakatumbula-Mratibu wa TASAF(W)</b>  Hakuna hatua zilizochukuliwa kutokana na hoja husika kusababishwa na	Hoja imefungwa			
--------------	--	---	---	---	----------------	--	--	--

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
		walengwa wa mpango katika muda muafaka	taarifa za walengwa wa mpango	kutoletwa kwa fedha				
2.3	<b>USIMAMIZI WA MATUMIZI</b> <b>Kiasi cha Tshs 3,044,000/= ambazo ni faini wanazokatwa walengwa kwa ajili ya kutotimiza masharti ya Afya na Elimu wakati wa kupitia Malipo ya wanufaika ilibainika kiasi cha adhabu zilizokatwa kwa wanufaika kwa kutotimia masharti ya afya na elimu kipo juu kutokana na wawezeshaji wa eneo la utekelezaji kutotoa elimu ya kutosha kuhusu haya masharti ya elimu na afya ili walengwa waelewe umuhimu wa kuwapeleka watoto wao kliniki na kuhudhuria masomo shuleni</b>	<b>Ushauri Na.2</b> Tunashauri uongozi wa wilaya ya Rungwe kutoa elimu ya kutosha kwa walengwa na umuhimu wa kuwapeleka watoto kliniki na watoto kuhudhuria masomo shuleni	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi, ni kweli fedha hizo zilikatwa kwa kutofauta vigezo vya masharti ya afya na elimu. Menejimenti imehakikisha elimu imetolewa kwa jamii kuhusu masuala ya afya na elimu na kwa sasa kaya zina mwitikio mkubwa	<b>Lydia Mwakatumbula-Mratibu wa TASAF(W)</b>  Mratibu alielekezwa kupitia kikao cha CMT cha tarehe 5 machi 2020 juu ya kutoa Elimu kwa walengwa kwa maswala ya Afya na elimu ili kukidhi vigezo vya masharti.	<b>Hoja imefungwa</b>			
2.3.2	<b>Kiasi cha Tshs 2,210,000 hazijalipwa kwa walengwa wa cash - plus wala hazijarudishwa TMU Mkaguzi baada ya kupitia hati ya malipo (PV) na taarifa ya TMO na payrolls zao walengwa wa CASH - PLUS, imeonekana</b>	<b>Ushauri Na.3</b> Tunashauri Menejimenti ya halmashauri kuongeza usimamizi na ufuutiliaji karibu kwa TOT na	Tunakubaliana na ushauri wa mkaguzi  Jumla ya Tshs 2,210,000 ambazo zilionekana haziklipwa kipindi cha ukaguzi ni kwa sababuu taarifa za malipo kwa walengwa zilikuwa bado hazijakusanywa kutoka vijijini kwa sasa taarifa	<b>Lydia Mwakatumbula-Mratibu wa TASAF(W)</b>  Mratibu wa TASAF alielekezwa kupitia kikao cha CMT cha	<b>Hoja imefungwa</b>			

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
	<p>Tshs 2,210,000 hazijalipwa kwenye vijiji 7 na hazijarudisha ofisini na T.O.T. Baadhi ya walengwa hawakuonekana kwenye payroll kwenye vijiji 4 ambaao thamani yake ni Tshs 782,000, kiasi cha shs 408,000 hakijasainiwa na walengwa kwenye Viji 3.</p> <p>Pia shs 3,160,000.00 walisaini vijana walengwa lakini wazazi kama wadhamini wao hawakusaini katika vijiji 8.</p> <p>Pia katika ukaguzi wa vijijini tarehe 01.10.2019 katika kijiji cha Ijoka mlengwa Ombeni E. Mwakyabara (12040610309605-T) na Robert Mwamonde (12040610309679-T) walishahama kwenda Dar -es-salaam wakati wamechukua hela shs,102,000.00 na mwagine shs 68,000.00</p>	<p>kuhakikisha fedha ambayo hajjalipwa inarudisha kwa wakati</p> <p>b. Timu ya ufuatilaji ihakikishe fedha ambazo hajjalipwa zinarudisha</p>	<p>zote toka vijijini zimekusanywa na zimeambatanishwa na majibu haya kwa ajili ya uhakiki. Pia walengwa ambao hawakuonekana kwenye payroll ambayo ni jumla ya Tshs 1,700,000.00 walikuwa hawajaonekana ni kwa sababu walikuwa wamechelewa kuja za mipango yao ya biashara, lakini baadaye walijaza na kwa sababu walikuwa hawamo kwenye payroll ya mwanzo hiyo TOTs wakati wa kulipa walishauriwa waandike majina yao kwa mkono wakati huo wakiwa vijijini na kuwalipa. Hata hiyo barua za watendaji wa vijiji kwa ajili ya udhibitisho zaidi wa haya malipo ziliandikwa barua za watendaji zimeambatanishwa na majibu haya.</p> <p>Kiasi cha Tshs 408,000.000 kutoka vijiji 3 ambacho hakikusainiwa na vijana walengwa lakini wazazi wao na wasimamizi wao waliwachukulia hizo fedha mbele ya ushahidi wa uongozi wa vijiji na TOTs kudhibitisha zaidi kwa</p>	<p>tarehe 05.03.2020 kuwa na usimamizi na ufuatilaji dhabiti kwa TOT na kuhakikisha fedha ambayo hajjalipwa inarudisha kwa wakati</p>				

NA/ PARA	HOJA YA UKAGUZI	MAPENDEKEZO YA MKAGUZI	MAJIBU YA UONGOZI	JINA/CHEO NA HATUA ZA KINIDHAMU ZILIZOCHUKULIW A KWA WAHUSIKA WALIOSABABISH A KUTOKEA KWA HOJA	MAONI YA MKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA UKAGUZI	MAONI YA KAMATI YA FEDHA	MAONI YA BARAZA LA MADIWANI
